

**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**  
**SHULE YA FANI NA SAYANSI ZA KIJAMII**  
**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIASILI.**

MATUMIZI YA SITIARI KATIKA VITENDAWILI VYA ABANYALA (k): MTAZAMO  
LINGANISHI NA VITENDAWILI VYA WASWAHILI.

BARASA MEBLE

C50/CE/11911/2007.

*Inakusudiwa kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika  
chuo kikuu cha Kenyatta.*

**KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY**

UNGAMO.

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijawahi kuwasilishwa kwa madhumni yoyote katika chuo kikuu kingine.

Mtahiniwa

Barasa

30.01.2014

Sahihi

Tarehe

Barasa Meble.

C50/CE/11911/2007.

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi waliochaguliwa na chuo kikuu cha Kenyatta.

Watahini

[Signature]

07-02-2014

Sahihi

Tarehe

Dkt. Edwin Masinde.

Idara ya Kiswahili na Lugha za Kafrika.

Barasa

7.2.2014

Dkt. Pamela Y. M. Ngugi.

Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika

## TABARUKU

Kwa wanangu Eugene, Daisy na Faith.

## SHUKRANI

Kazi ya kuushughulikia utafiti huu ilikuwa ngumu na iliyohitaji subira kubwa. Kazi hii isingefanyika bila ya kuwako kwa msaada wa watu wengine. Msaada huo ulikuwa wa kila aina, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na uwezo wa kushughulikia yote yaliyohitajika kwenye utafiti huu. Pili nampongeza mamangu Grace Barasa kwa kunishajiisha kila mara kukamilisha shughuli hii. Mama jitihada zako hazikuambulia patupu.

Sitawasahau wasimamizi wangu Dkt. Edwin Masinde aliyenielekeza ipasavyo mambo yalipokaribia kwenda upogo, bila kumsahau Dkt. Pamela Ngugi aliyekuwa tayari kunisikiliza na kunipa mwelekeo nilipokaribia kuugonga mwamba. Shukrani zangu pia ziwaendee wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili kwa mwongozo walionipa wakati wa kulitetea pendekezo langu la utafiti.

Wanafunzi wenzangu ambao tulikuwa nao pia wanastahili shukrani za kipekee. Tulisaidiana kupanda hadi ngazi za juu. Mlinisaidia kwa kunipa moyo wakati nilizidiwa na kazi. Hawa ni pamoja na Regina, Birir, Helena, Elizabeth, Sophie na wengine ambao sijawataja hapa. Mme wangu Evans Omwando pamoja na wanangu Eugene, Daisy na Faith, nawatolea shukrani zangu za dhati kwa msaada mlionipa wakati huo mgumu.

## MAELEZO YA MSAMIATI.

*Ebikiye bie moni* – limetumiwa katika utafiti huu kwa maana ya kope za macho.

*Enjukhi* – mdudu mwenye mbawa nne anayeweza kuuma, anayeishi katika makundi kwenye mzinga na hutengeneza asali na nta; nyuki.

*Enyimba* – ni kengele ndogondogo zinazofungwa miguuni, mikononi wakati watu wanapocheza ngoma au watoto waanzapo kutembea. Kwenye utafiti huu, neno hilo limetumiwa kwa maana ya kengele za mikono wanazocheza vijana wanapojiandaa kwa sherehe za kupashwa tohara; njuga.

*Esisieno* – malaika anayesadikiwa kuwa amelaaniwa kwa kukataa kufuata amri za mwenyezi Mungu; ibilisi, milihoi, shetani.

*Namunyu* – jitu, kwenye utafiti huu neno hilo lilitumiwa kwa maana ya ugonjwa wa Ukosefu Wa Kinga Mwilini (UKIMWI).

*Owusuma* – chakula kilichopikwa kutokana na unga wa mahindi ama mtama kwa kusongwa; sima

## IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza matumizi ya sitiari katika vitendawili vya jamii ya Abanyala na Waswahili. Mtafiti alichochewa na hali kwamba hata kama waandishi wa vitendawili walifanya kazi kubwa kuhusu kuvikusanya, kuviainisha, kueleza sifa na dhima yavyo, swala la matumizi ya sitiari katika vitendawili halijashughulikiwa hasa katika jamii zilizolengwa. Sitiari ni mojawapo ya mbinu muhimu inayotumiwa katika uundaji wa vitendawili. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Semiotiki iliyoasisiwa na mwanaisimu wa Ki-Swizi Ferdinand de Saussure aliyeiwekea misingi katika mwaka wa 1906. Baadaye iliendelezwa na Charles Peirce na Roland Barthes ambao walikuwa na mtazamo tofauti na Saussure. Utafiti huu ulizingatia mtazamo wa C.R. Peirce na Barthes ambao ulimwezesha mtafiti kushughulikia ishara hususan ishara picha, ishara kamili ( elekezi ), taashira na ishara tanakali. Nguzo za nadharia hiyo zilizoongoza utafiti huu ni msimbo wa matukio, kihemenitiki, kiseme, kiishara, na kirejelezi. Zilimwezesha mtafiti kufasiri sitiari zilizo katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Kueleza maudhui katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Pia zilimwezesha kuchunguza kwa nini Abanyala na Waswahili hutumia vitendawili katika mawasiliano yao. Utafiti huo ulifanywa maktabani kwa kusoma majarida, vitabu na tasnifu kuhusu sitiari na vitendawili. Aidha utafiti ulifanywa nyanjani ambapo data ambako data kuhusu vitendawili ilifanywa kwa kutumia hojaji, uchunguzi ushiriki na mahojiano. Uteuzi wa sampuli kimaksudu ulitumiwa kwa misingi ya tajriba na maarifa ya jamii lengwa. Kwa hivyo watoto watano wa darasa la sita, ajuza watano na wazee watano waliteuliwa. Uchanganuzi wa data ulifanya kwa kuzingatia maswali, malengo na mihimili ya nadharia. Matokeo yaliwasilishwa kwa mjia ya maelezo na mifano. Data iliwasilishwa katika sura tano. Sura ya kwanza utangulizi. Sura ya pili aina za sitiari zilibainishwa katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Sura ya tatu imeshughulikia maudhui katika vitendawili. Sura ya nne ilishughulikia sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili. Sura ya tano ilishughulikia matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo. Utafiti huu utakuwa wenye manufaa kwa wakuzi mitaala, wahakiki wa fasihi na jamii kwa ujumla

## ABSTRACT

The purpose of the study is to investigate the use of metaphor in the Abanyala and Swahili riddle. The researcher was inspired by the fact that even though the writers and researchers of riddles did a lot in collecting, classifying and giving functions of riddles, the aspect of the use of metaphor in riddles was overlooked. More so in the specified communities. Most riddles are in fact metaphors for this reason the researcher looked into the use of the metaphor in the Abanyala and Swahili riddle. The researcher based on the principles laid out in the Semiotic Theory which was found by Ferdinand de Saussure in the year 1906. The theory was later developed by Charles Pierce and Roland Barthes who had a different view from Ferdinand de Saussure. Pierce and Barthes associated sign and meaning in relation to the context. Pierce believed that sign as an object, can be classified as an icon, an index, or a symbol. Barthes is associated with the code which he believes that it can be used in analyzing literature, he further divided the code as follows: proairetic, hermeneutic, semic, symbolic and referential codes. These principles were used in establishing types of metaphors in the Abanyala and Swahili riddles. The importance of metaphors in the Abanyala and Swahili riddles. The principles also guided the researcher in finding out why the Abanyala and Swahili use riddles. The research started from the library in which information pertaining riddles and metaphors were found. Thereafter the researcher went into the field for data collection. Purposive sampling was used during data collection whereby five standard six pupils in five primary schools, five old men and five old women were sampled basing on their knowledge and experience in the targeted community. Questionnaire, discussion and observation methods were used during data collection. The research report is divided into five chapters. Chapter one deals with introductory issues. Chapter two deals with types of metaphors used in Abanyala and Swahili riddles. Chapter three metaphors and their uses, chapter four why the Abanyala and Swahili use riddles. Chapter five conclusions research findings and recommendations. The findings of the study will benefit the society as a whole.

## **YALIYOMO**

Ungamo.....	ii
Tabarurku.....	iii
Shukrani.....	iv
Maelezo ya maneno.....	v
Ikisiri.....	vi
Abstract.....	vii
Yaliyomo.....	viii

## **SURA YA KWANZA**

1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Usuli.....	1
1.2 Suala la utafiti.....	4
1.3 Maswali ya utafiti.....	4
1.4 Malengo ya utafiti.....	5
1.5 Sababu za kuchagua mada.....	5
1.6 Upeo na mipaka.....	6
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada.....	7
1.7.1 Maandishi kuhusu vitendawili .....	8
1.7.2 Matumizi ya lugha katika vitendawili .....	13
1.7.3 Yaliyoandikwa kuhusu sitiari.....	14
1.8 Misingi ya kinadharia.....	17

1.9 Mbinu za utafiti.....	24
1.9.1 Sampuli lengwa.....	25
1.9.2 Njia na vifaa.....	25
1.9.3 Uchanganuzi wa data.....	26
1.9.4 Uwasilishaji wa data.....	26

**SURA YA PILI : AINA ZA SITIARI ZINAZOBAINIKA KATIKA**

**VITENDAWILI VYA ABANYALA NA WASWAHILI**

2.0 Utangulizi.....	27
2.1 Sitiarifiche.....	28
2.2 Sitiari shehenezi.....	32
2.3 Sitiari Tashhisi.....	35
2.4 Sitiari Thabiti.....	39
2.5 Sitiari Changanyi.....	42
2.6 sitiari Changamano .....	44
2.7 Sitiari Dhanifu.....	45
2.8 Hitimisho.....	47

**SURA YA TATU: MAUDHUI KATIKA VITENDAWILI VITENDAWILI VYA**

**ABANYALA NA WASWAHILI**

3.0 Utangulizi.....	49
3.1 Sitiari kama kiashirii cha ugonjwa na kifo.....	49
3.2 Sitiari kama kiashirii cha mifumo ya kihistoria iliyoshuhudia majilio ya wageni.....	52
3.3 Sitiari kama kiashirii cha sayansi ya kimazingira.....	56

3.4 Sitiari kama kiashirii cha mchapuko wa teknolojia.....	58
3.5 Sitiari kama kiashirii cha chakula.....	60
3.6 Hitimisho.....	63

**SURA YA NNE: DHIMA YA VITENDAWILI KATIKA JAMII ZA ABANYALA NA WASWAHILI**

4.0 Utangulizi.....	65
4.1 Kitendawili kama chombo cha kuchochea udadisi.....	65
4.2 Kitendawili kama chombo cha kukuza maadili.....	68
4.3 Kitendawili kama chombo cha kuelimisha.....	70
4.4 Kitendawili kama njia ya kudhihaki.....	73
4.5 Kitendawili kama kigezo cha kusawiri maisha ya jamii.....	74
4.6 Kitendawili kama chombo cha kuburudisha.....	77
4.7 Kitendawili kama mbinu ya kuwasilisha muhtasari wa ujumbe.....	78
4.8 Hitimisho.....	78

**SURA YA TANO: HITIMISHO**

5.0 Utangulizi.....	81
5.1 Muhtasari .....	81
5.2 Matokeo ya utafiti .....	81
5.3 Mchango wa utafiti .....	88

5.4 Changamoto za utafiti.....	88
5.5 Mapendekezo.....	89
5.6 Hitimisho.....	89
<b>MAREJELEO</b> .....	91
<b>VIAMBATISHO</b> .....	97
(i) Kiambatisho cha maswali ya mahojiano kwa wazee wa jamii ya Abanyala .....	97
(ii) Kiambatisho cha maswali ya mahojiano kwa wazee wa jamii ya Waswahili .....	98
(iii) Kiambatisho cha maswali ya mahojiano kwa watoto .....	99
(iv) Kiambatisho cha eneo la Abanyala (k) .....	100
(v) Kiambatisho cha eneo la Mombasa Mji wa Kale.....	101

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Katika sura hii utafiti unalenga kujadili vipengele vya kimsingi vya utafiti. Vipengele vitakavyojadiliwa ni kama vile: usuli wa utafiti, swala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya kinadharia na mbinu za utafiti miongoni mwa vingine.

### 1.1 USULI

Vitendawili ni kipera cha utanzu wa semi wa fasihi simulizi. Wamitila (2003) anaeleza semi kuwa ni fungu la tungo za fasihi simulizi ambazo ni fupi fupi na zina matumizi ya taswira, tamathali na ishara kwa mapana. Msokile (1993), anaeleza kitendawili kuwa ni maneno yanayoficha maana ya kitu ili kisijulikane kwa urahisi. Nao King'ei na Kisovi (2005) wanaeleza vitendawili kwamba ni aina ya mafumbo ambayo aghalabu hufumbuliwa kwa neno moja. Kwa hivyo, vitendawili ni mafumbo ya maneno ambapo vitu na hali ya kawaida huelezwa kipicha ili hadhira iweze kung'amua kinachosemwa. Fumbo lenyewe na jibu lake, hufahamika katika jamii fulani ambayo huliwasilisha fumbo lenyewe kama swali au kauli. Vitendawili ni zao la jamii mahsusi yenye utamaduni, lugha na mazingira mahsusi. Kama sanaa ya kifasihi, vitendawili haviwezi kuepuka athari za kitamaduni na kimazingira. Jambo hili limevifanya kusheheni lugha ya kipicha inayotumia ishara na inayoeleweka kimaana na kimatumizi ndani ya utamaduni na mazingira yanayoviibua.

Vitendawili hutekeleza majukumu muhimu katika jamii, dhamira yake ikiwa ni kuupanua ujuzi wa hadhira kuhusiana na mazingira yake pamoja na kuukuza wepesi wa kuwaza, kufikiri na kuchemsha bongo. Sanaa hii hutegemea uwezo wa hadhira kuweza kutambua,

kuhusisha, kulinganisha, kulinganua na kufumbua vilivyoko katika mazingira yake. Wengi wa wataalam waliochunguza vitendawili, wanadai kwamba madhumni makuu ya vitendawili ni mchezo wa kuburudisha watoto; (Blacking 1961). Hata hivyo mchezoni watoto hujifunza mengi kwa mfano huwatayarisha kutambua mambo kadha katika matumizi ya lugha yakiwemo sitiari na utata. Nakunga (2011), anaeleza kuwa sitiari hazifundishwi kwa kuoneshwa bayana kwa watoto kwamba hii ni sitiara na maana yake ni hii lakini kwa kutega na kutegua vitendawili kwa muda mrefu, wanaweza kutambua kuwa maneno mengine huweza kumaanisha kitu kingine katika mawanda tofauti kabisa.

Sifa za matumizi ya mbinu za kitamathali hudhihirika katika muundo wa vitendawili. Mbinu za kitamathali aghalabu huhusiana na maana na maudhui ya vitendawili. Mbinu hizi hutumiwa kuupa muundo wa vitendawili urembo na kuifanya maana yake iwasilishwe kwa njia inayovutia. Miongoni mwa mbinu hizo za kitamathali ni sitiari.

Msokile (1993) anafafanua sitiari kama tamathali ya usemi inayolinganisha na kuhusisha vitu vilivyo tofauti kitabia na kimaumbile. Anaeleza zaidi kwamba ni tamathali ambayo athari yake hutegemea kuhamishwa kwa maana na hisi kutoka katika kitu kimoja na kwenda katika kitu kingine. Sitiari hutawala katika umbo la vitendawili na hutoa taswira za vitu, wazo, dhana au maumbile katika mazingira maalum na kwa wakati maalum Momanyi (2006). Pia uteuzi wa sitiari katika vitendawili, hutoa sifa ya kukejeli na kuwadhihaki watu fulani kwa kuyatumia majina yao kama msingi wa ulinganishi kwenye muundo wa vitendawili husika.

Vitendawili vilikusudiwa kupima kumbukumbu za watoto. Farsi (1979) analiunga mkono wazo hili kwa kusema kuwa hali hiyo iliwafanya wazee kuwaacha watoto wapigiane

vitendawili wao wakiwa wasikilizaji na waamuzi. Kwa njia hii, watoto, vijana na hata wazee walijifunza amali nyingi za jamii zao.

Mbali na hayo vitendawili hutumia majina ya vitu vilivyo katika mazingira ya jamii fulani. Hali hii huwafunza wale wanaotegeana vitendawili majina na mambo mbalimbali ya kimazingira. Miruka (1994) anakubaliana na jambo hili kwa kukiri kuwa njia hiyo hurahisisha uelewa wa hali ya maisha ya jamii yoyote kupitia kwa vitendawili vyao.

Umbo la vitendawili limejikita katika mfumo maalum unaohusisha swali na jibu. Muundo kama unavyoelezwa na Nakunga (2011), ni jumla ya uhusiano unaokuwako kati ya visehemu mbalimbali vinavyotengeneza kitu kamili, hivyo basi katika vitendawili, muundo ni utaratibu unaofuatwa wakati wa kutega na kutegua kitendawili. Utaratibu huo huanza kwa kiingizi au kitangulizi kinachotanguliza kwa swali ambacho hutangaza majilio ya kitendawili. Kikaribisho ambacho ni jibu hutoka kwa hadhira ambayo ni ishara ya kukubali kwao kutegewa kitendawili. Baadaye mwili wa kitendawili hutolewa na huhitaji jibu kutoka kwa hadhira.

Mazungumzo mengi husheheni matumizi ya sitiara. Jamii ya Abaluyia kama anavyodai Kobia (2008) hutumia sitiari ili kuficha aibu iliyo katika baadhi ya maneno. Jamii hiyo huamini kuwa maneno ambayo ni mwiko, hayastahili kusemwa hadharani. Vilevile Gibbs (1994) anakiri kwamba sitiari zinaweza kutumiwa kueleza mada ambazo haziwezi kuelezeka kwa njia ya moja kwa moja. Mbali na hayo Todoli (2007), anasisitiza kuwa sitiari zinaweza kutumiwa kueleza mambo mazito na yakawa mepesi kwa njia isiyoudhi mtu yeyote. Hali hiyo hufikiwa kwa kutumia ishara au picha ambazo zinafahamika na kueleweka kwa umma.

Baadhi ya sitiari hizo, ndizo zinazotumiwa katika uundaji wa vitendawili vya Abanyala na Waswahili.

Sitiari zinazotumiwa na jamii ya Abanyala na Waswahili huwa na maana nyingi. Vilevile sitiari tofauti zinaweza kuwa na maana sawa. Kwa hivyo ufahamu wa kina kuhusu sitiari fulani unafaa kufanywa kabla ya kukubali maana yake. Utafiti huu unadhamiria kubainisha sitiari zilizo katika vitendawili vya jamii ya Abanyala na Waswahili, umuhimu wa sitiari katika vitendawili vya jamii lengwa. Pia unanua kuchunguza sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao.

## **1.2 SUALA LA UTAFITI**

Katika utamaduni wa Abaluyia na Waswahili, kuna njia nyingi za kuwasilisha ujumbe, njia mojawapo ni kupitia kwa vitendawili. Katika kuunda vitendawili, sitiari ni mojawapo ya mbinu kuu zinazotumiwa. Kwa hivyo utafiti ulinua kubainisha sitiari zilizo katika vitendawili vya Abanyala, maudhui yake, vile vile utafiti huu ulieleza sababu zinazowafanya Abanyala kutumia vitendawili katika mawasiliano yao kwa kulinganishwa na vitendawili vya Waswahili.

## **1.3 MASWALI YA UTAFITI**

1. Je, ni sitiari zipi zinazobainika katika vitendawili vya jamii ya Abanyala na Waswahili?
2. Je, sitiari zinazotumiwa katika vitendawili vya jamii ya Abanyala na Waswahili zina maudhui gani?
3. Kwa nini Abanyala na Waswahili hutumia vitendawili katika mawasilino yao?

#### **1.4 MALENGO YA UTAFITI**

1. Kubainisha sitiari zilizo katika vitendawili vya jamii ya Abanyala na Waswahili.
2. Kubainisha maudhui katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili.
3. Kueleza sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao.

#### **1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA**

Baadhi ya wanafasihi wametoa mwito wa kudhibiti na kushabikia simulizi zetu. Kwa mfano P'Bitek (1973), anaona kwamba upo umuhimu wa kufurahia fasihi zetu za Kiafrika hasa katika mawanda ya kielimu malengo yakiwa ni kuwafanya wanafunzi wafaulu mtihani, waburudishwe na kuisimuliwa na sanaa hii hasa vitendawili. Lo Liyong akinukuliwa na Chacha (1991), anasisitiza zaidi kuwa tutambue majukumu yanayoweza kutekelezwa na amali za kiasili kwa manufaa ya jamii ya leo. Kwa hivyo vitendawili kama sehemu ya masimulizi yetu, ni amali muhimu za jamii basi hatuna budi kuviendeleza na kuvihifadhi.

Katika mafunzo ya shuleni na vyuoni, aina ya fasihi ambayo imekuwa ikifunzwa na kuisitizwa imekuwa fasihi andishi. Fasihi simulizi imekuwa ikipuuzwa mpaka miaka ya hivi karibuni. Hata hivyo bado kuna upungufu wa vitabu na majarida ya kuwasaidia walimu na wanafunzi. Tafiti za namna hii zikifanywa kwa wingi zitatoa mchango mkubwa sana kutimiza lengo hilo. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa hatujengi tu misingi imara ya elimu ya watoto wetu bali pia tutakuwa tunajenga uhai wa taifa kama anavyosema Chacha (1991).

Kama anavyosema Omari na wengineo (1975), tusipowafunza vijana wetu wanaosoma katika shule na vyuo amali hizi, hawa watakuwa wamepoteza urithi muhimu kwa hivyo mbali na kuwa kipera hiki hutahiniwa katika mitihani ya kitaifa ya darasa la nane na kidato cha nne,

utafiti huu utawafaidi walimu na wanafunzi kwa kupata uelewa zaidi wa utanzu huu mfupi wa fasihi simulizi.

Lugha ya Kiswahili imekuwa ni lugha ya taifa hapa nchini Kenya na tunapotafsiri fasihi za jamii za kiasili hadi kwenye lugha ya Kiswahili, hapo huwa zinakuwa sehemu ya fasihi simulizi ya Kiswahili. Kwa kufanya hivyo huwa hatuikuzi tu lugha ya Kiswahili bali pia tunajenga utamaduni wa taifa vile anavyoeleza Matheru (1983). Kwa hivyo, kipera hiki cha vitendawili kinafaa kushughulikiwa.

Momanyi (2006) anapendekeza kwamba utafiti unahitaji kufanywa ili kubainisha maumbo ya kitamathali yanayotumiwa kuundia vitendawili, anaeleza zaidi kwamba kuna baadhi ya hoja zinazotolewa kuwa sanaa ya vitendawili inaonyesha dalili za kudumaa na hakuna ithibati za kiutafiti zinazoonyesha mwelekeo na ukuaji wake hasa katika janibu zetu. Kwa hivyo utafiti huu unanua kutoa mchango wa kiusomi kwa uwanja huu mpana wa fasihi simulizi. Kwa mchango huu, mtafiti anatarajia kuziba pengo la ukosefu wa tafiti za kutosha kuhusiana na sehemu hii muhimu. Nia yake ni kutaka kutoa mchango wake kuongezea kwenye idadi ya tafiti zilizofanywa na zitakazofanywa kuhusu fasihi simulizi ambazo zitakuwa kumbukumbu na msingi kwa wataalam wengine kuanzisha utafiti mwingine.

Utanzu huu ni miongoni mwa mbinu zinazoshughulikia maswala ibuka katika jamii kama vile magonjwa yasiyo na tiba, uchumi na siasa. Hali hii imevifanya vitendawili kuwa njia maarufu ya mawasiliano (Kobia 2008). Kwa ufundi wake wa matumizi ya sitiari, wengi wameweza kujieleza hata jambo zito likaonekana kuwa jepesi. Kwa ajili hii kazi hii itakuwa yenye manufaa kwa wakuza mitaala, wahakiki wa fasihi, walimu, wanafunzi na jamii kwa ujumla.

Jamii za Abanyala na Waswahili hutumia vitendawili. Kwa hivyo kuna haja ya kubaini ulinganisho wa sitiari zinazotumiwa katika vitendawili vya jamii hizi mbili za Abanyala na Waswahili. Isitoshe kuna haja ya kutazama ulinganisho wa maudhui ya sitiari katika vitendawili vya jamii hizi. Ulinganisho huo ulitumiwa ili kurahisisha uelewa wa vitendawili kwa hivyo utarahisisha ufundishaji wake na lugha ya Kiswahili kwa ujumla (Trang 2013).

Vilevile Abanyala na Waswahili huishi katika mazingira tofauti. Kwa hivyo kulikuwa na haja ya kuona namna ambavyo mazingira tofauti huathiri matumizi ya sitiari katika vitendawili. Kwa sababu hii, mtafiti alilenga kubaini namna mazingira tofauti huzua aina tofauti za sitiari na maudhui tofauti katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili.

#### **1.6 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI**

Utafiti huu ulikita katika matumizi ya sitiari katika vitendawili vya jamii ya Abanyala wanaopatikana katika sehemu za magharibi mwa nchi ya Kenya jimbo la Kakamega na Waswahili wa Kenya hasa wa Mombasa mji wa Kale. Utafiti ulilenga kubainisha sitiari zilizo katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili; sitiari zilizoshughulikiwa katika utafiti unaotarajiwa ni: sitiari fiche, sitiari kale na sitiari shehenezi. Aina hizo za sitiari zinaelezwa na Msokile (1993) kama ifuatavyo : sitiari fiche anaifafanua kama tamathali ya usemi inayolinganisha vitu viwili kwa uhusiano wa mbali, wazo linalojitokeza huwa mbali kwa kawaida; sitiarififi au sitiari kale ama sitiari chakavu anaieleza kuwa ni sitiari iliyozeleka sana katika matumizi ya kawaida kiasi kwamba mtu hatambui kuwa ni tamathali ya kisitiari. Vilevile kuna sitiari shehenezi ambayo huongoza maana na sifa za neno linalolinganishwa. Umuhimu wa sitiari hizo katika vitendawili vya jamii ya Abanyala na Waswahili ni jambo

ambalo mtafiti alitilia maanani. Fauka ya hayo, utafiti wake ulijikita kwenye sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao.

Mtafiti alitumia jamii ya Abanyala kama kielelezo cha jamii ya Abaluyia na jamii ya Waswahili wa Mombasa Mji wa Kale kama kielelezo cha jamii ya Waswahili. Mtafiti anavyoona, jamii ya Abanyala na Waswahili zilitosheleza kupitia kwa utafiti awali ulioonyesha kwamba kuna data ya kutosha.

## **1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA**

Utafiti huu unazingatia vitendawili na sitiari kwa hivyo yaliyoandikwa kuhusu mada hii ya utafiti yamegawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza itashughulikia yaliyoandikwa kuhusu vitendawili na matumizi ya lugha katika vitendawili. Sehemu ya pili itashughulikia yaliyoandikwa kuhusu sitiari.

### **1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu vitendawili**

Kuna mengi yaliyoandikwa kuhusu vitendawili walakini siyo mengi yaliyoandikwa kuhusu matumizi ya sitiara katika vitendawili. Wamitila (2003), anaeleza kuwa kitendawili ni aina ya semi ambazo huwa zimefumbwa na hutolewa kwa hadhira au mtu ili azifumbue. Kinge'i na Kisovi (2005), nao wanaeleza kitendawili kuwa aina ya mafumbo ambayo aghalabu hufumbuliwa kwa neno moja. Kwa hiyo, vitendawili ni mchezo wa kuficha maana; utandu wa maneno ambamo dhana husimuliwa kiisitiari ili mtu mwingine ang'amue.

Wataalamu wengi wameshughulikia vitendawili, wataalam wa mwanzo kujishughulisha na uchunguzi wa vitendawili vya jamii za Kiafrika walikuwa Wamishenari, wanaathropolojia, wanaisimu na wanafasihi kwa mfano Finnegan (1970) utafiti wake ulizingatia jamii za kusini

mwa Afrika uliobainisha kuwa fasihi simulizi ni zao halisi la utamaduni maalum na kuwa si vyema kuushughulikia utanzu wowote nje ya utamaduni wa jamii inayohusika. Mtaalam huyo anasisitiza kuwa dhima ya vitendawili ni kuburudisha kuliko kuelimisha na ndio maana anaona vitendawili kuwa ni jambo la kitoto kwa hivyo visiingaliwe kwa makini. Mawazo hayo yalimfanya mtafiti kuona kwamba ipo haja ya kujua sitari zinazobainika katika vitendawili na umuhimu wa sitiari hizo kwa kurejelea jamii ya Abanyala na Waswahili.

Uchunguzi wa Beuchat (1965) katika vitendawili ulijikita zaidi kwenye misingi ya kiisimu. Baada ya kuziangalia sifa na sura mbalimbali kuhusu vitendawili; anatoa kauli kuwa lengo kuu la vitendawili ni kuburudisha na ndio maana hupigwa magharibi baada ya kazi ama mihula isiyo ya kazi. Hata ingawa uchunguzi huo unahusu vitendawili, tofauti na huu ni kwamba utafiti huu uliangalia matumizi ya sitiari katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili.

Nandwa (1976) alifanya utafiti na uchunguzi katika fasihi ya Waluyia, anaeleza kuwa miongoni mwa jamii ya Waluyia, vitendawili huchukuliwa kama ni mchezo wa watoto unaowaburudisha. Jambo lililo wazi ni kuwa utafiti huo unaeleza mengi kuhusiana na dhima ya vitendawili katika jamii tofauti na ilivyo katika utafiti huu kwani ulilenga kubaini sitiari na umuhimu wake katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Hata hivyo utafiti huo ulimfaa mtafiti kueleza sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao.

Vitendawili vya jamii mbalimbali katika eneo la kusini mwa Afrika, vimechunguzwa na Hamnet (1967). Uchunguzi wake uliegemea zaidi kwenye dhima ya vitendawili, alieleza jinsi vitendawili huweza kutumiwa kutanua akili za wasikilizaji na kutoa mafunzo mbalimbali juu

ya maisha. Alieleza hata tafsiri ya kicheko kinachofuata jawabu na kusema kuwa mbali na kuwa futuhi, kicheko hicho huwa kinaajabia usanii na ubunifu katika kitendawili hicho. Kazi hiyo ilitofautina na utafiti huu kwani mtafiti alitazama sitiari na umuhimu wake katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Hata hivyo mtafiti alinufaika kutokana na maelezo hayo kwa kuchunguza sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao.

Kipury (1983) alifanya uchunguzi kuhusu vitendawili vya Wamaasai, katika kazi yake, ameeleza umuhimu wa vitendawili na kuviainisha kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: watu, uundaji wa nyumba, utamaduni, mazingira, mimea, wanyama na wadudu. Katika uainishaji huo, ametolea kila kipengele mifano ya vitendawili kutoka jamii hiyo ya Wamaasai. Kazi hiyo inatofautiana na utafiti huu kwani swala la sitiari katika vitendawili, hakulishughulikia, cha mno ni kuwa kazi zote zinashughulikia vitendawili.

Vitendawili vya jamii ya Agikuyu vimeshughulikiwa na Kabira (1988) ambaye alitoa mifano ya vitendawili vya jamii hiyo kisha akaitafsiri katika lugha ya Kiingereza. Vile inavyodhihirika, swala la matumizi ya sitiari na umuhimu wake katika vitendawili hasa katika jamii ya Abanyala na Waswahili, bado halijashughulikiwa.

Kazi ya Chesaina (1991) kuhusu vitendawili vya Wakalenjin vilevile inatofautina na utafiti unaotarajiwa kwa sababu mtaalam huyu alijihusisha na uainishaji wa vitendawili vya jamii hiyo akirejelea ndege, mimea, matukio ya kawaida, sehemu za mwili na teknolojia ya kisasa. Alitolea vitengo hivyo mifano kutoka jamii hiyo kisha akaitafsiri katika lugha ya Kiingereza. Hata hivyo uchunguzi huo ulimfaa mtafiti kwa kuchunguza sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao.

Miruka (1994), ametoa mchango wake kuhusu kitengo hiki cha vitendawili kwa kuvianisha kwa misingi ya mambo tofauti, pia ameonyesha utendaji katika vitendawili isitoshe ameonyesha dhima ya vitendawili katika jamii kwa kueleza kuwa maudhui ya vitendawili hudhibitiwa na hutegemea mazingira ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na hata kitamaduni ya jamii inayohusika. Ndio maana ni rahisi kuelewa jamii inajihusisha na shughuli gani na imepita kwenye mifumo ya aina gani. Mawazo haya yalimfaa mtafiti katika kuchunguza maudhui katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili ili kupata uelewa wa hali ya maisha ya jamii lengwa ijapokuwa utafiti huo ulitofautiana na huu.

Wasomi wengine walioshughulikia vitendawili ni kama vile Harries (1942) aliyekusanya vitendawili vya Makua. Farsi (1958) na Lambert (1962/3) wakakusanya vitendawili vya jamii ya Waswahili. Ukusanyaji huo ni dhihirisho tosha kuwa swala la sitiari katika vitendawili bado halijashughulikiwa.

Mbaabu (1978), alifafanua mambo na vitu vinavyotajwa kwenye sehemu ya swali la kitendawili (kisabiki) katika misingi ya utamaduni wa jamii ya Wameru. Maelezo hayo yalimpa mtafiti changamoto ya kuchunguza ubunifu ulio katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili kwa kuzingatia kipengele cha sitiari katika vitendawili vya jamii lengwa.

Utafiti wa Ngonyani (2005), kuhusu “Vitendawili vya Kiswahili: Usambamba wake na Dhima yake katika Jamii,” alishughulikia mada hiyo kwa kuchambua mfanano wa muundo wa sentensi na usambamba wa kifonolojia, kisémantiki na kisintaksia katika kisabiki. Alibainisha kwamba usambamba huo ndio asili ya sitiari na sitiari hizo, ndizo zinazotumiwa katika kuunda mafumbo ya vitendawili. Aligundua kwamba kisabiki hutoa maneno yanayohusu mawanda chanzo na maneno yanayoonekana katika mawanda yalengwayo.

Vilevile nyongeza ndizo hufanywa ili kuonyesha kwamba ingawa kuna usambamba wa maneno katika mawanda mawili, kuna sifa au maneno ambayo si sahihi kwa mawanda yalengwayo. Utafiti huo unakaribiana na huu ingawaje utafiti huu ulibaini sitiari zilizo katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili pia umuhimu wa sitiari hizo ulichunguzwa.

Momanyi (2006), alitafiti “Dhima na Utendakazi wa Vitendawili katika Jamii,” alitambua kwamba vitendawili hubadilika kutegemea wakati vivyo hivyo vikatumiwa kama hati za kihistoria, vikawa kumbukumbu ya mambo na matendo ambayo huenda yamebadilika au kuachwa nyuma na wakati. Isitoshe alitambua kuwa vitendawili vina jukumu la kufunza sayansi ya kimazingira na utamaduni kwa hivyo vikatoa mwelekeo wa maisha kwa jamii husika. Vilevile alitambua kuwa vitendawili huweza kufunza mienendo na kanuni zinazokubalika katika jamii mbali na kusawiri maisha ya jamii. Alifafanua dhima hizo kwa kutoa mifano mbalimbali ya vitendawili. Tofauti na utafiti huu ni kwamba utafiti huu ulitazamia kubaini sitiari na umuhimu wake katika vitendawili ingawaje utafiti huo wa Momanyi (2006) ulimfaa mtafiti kuchunguza sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao.

Chacha (1991), ameshughulikia maana na matumizi ya vitendawili vya jamii ya Wakuria kwa kuangalia sura na sifa mbalimbali zinazotambulisha vitendawili kama utanzu maalum na wenye umuhimu mkubwa katika fasihi simulizi. Amebainisha kwamba vitendawili vina sifa maalum ya kutumia lugha iitwayo sitiara zinazotolewa kwenye mazingira yanayohusika na huweza kueleweka vyema kimaana na kimatumizi katika utamaduni na mazingira hayo. Utafiti huo unakaribiana na huu kwa vile unahusu vitendawili, hata hivyo tofauti ni kwamba, utafiti huu ulilenga matumizi ya sitiara katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Chamo ni kuwa tafiti zote mbili zililenga vitendawili.

Tafiti zilizodondolewa na kupitiwa katika udurusu wa mtafiti, zilimfaa kwa kumwelekeza katika utafiti wake huku akilijaza pengo lililoachwa la matumizi ya sitiara katika vitendawili vya Abanyala vikilinganishwa na vya Waswahili.

### **1.7.2 Matumizi ya lugha katika vitendawili**

Kuhusu matumizi ya lugha katika vitendawili, Pensinger (2001) anaeleza kwamba swala la matumizi ya lugha katika vitendawili lilishughulikiwa mwanzoni na Aarne – Thompson aliyeainisha vitendawili kwa kutegemea muundo. Maelezo haya yalikuwa muhimu kwa utafiti wetu kwa ambavyo yalituwezesha kuzingatia kipengele cha matumizi ya sitiari katika jamii za abanyara na waswahili.

William R. Bascom (1949) alishughulikia matumizi ya lugha katika vitendawili vya Wayoruba. Alipendekeza tafiti zaidi zifanywe kuhusu muundo na fani. Hii ndiyo maana Kazi hii ilimwezesha mtafiti kushughulikia sitiari na matumizi yake katika vitendawili vya jamii za Abanyala na Waswahili.

Scott (1965) aliangalia fani na namna zinavyojitokeza katika vitendawili vya Waarabu. Ni kutokana na kazi hii ndipo utafiti wetu ulichagua matumizi ya sitiari kama mojawapo ya vipengele vya fani na kuangalia matumizi yake katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili.

Wamitila (2003) ameonyesha matumizi ya lugha katika vitendawili kwa ujumla. Amefafanua fani mbalimbali zinavyojitokeza katika vitendawili. Baadhi ya fani hizo ni kama vile methali, tashbihi, tashhisi, kejeli, tanakali za sauti, sitiari miongoni mwa fani zingine. Hata hivyo sehemu inayohusu sitiara haikushughulikiwa kwa mapana. Ameeleza jinsi ambavyo sitiari

zinatumiwa kuunda vitendawili. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwa sababu utafiti wetu ulishughulikia sitiari na maudhui katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili.

Amana (2013), ameshughulikia asili ya vitendawili, sifa, muundo wake, aina na fani katika vitendawili. Ameshughulikia baadhi ya vipengele vya fani kama vile tashhisi, kwelikinzani, takriri na sitiari. Ingawa kazi yake pia ilihusu sitiari ametoa mifano, kazi yake ni tofauti na yetu iliyolenga kubaini aina za sitiari na maudhui ya vitendawili katika jamii teule.

Trang (2013) aliangalia matumizi ya lugha katika vitendawili vya Kiingereza na Kivietnamu. Kwamba matumizi hayo hutokea ili hadhira iweze kuwaza na kuwazua kuhusu kile kinachosemwa. Isitoshe aliangalia mlingano na mlingano wa lugha inayotumiwa katika vitendawili vya lugha hizo mbili. Utafiti huo ni tofauti na wetu kwa sababu utafiti huu umeangalia aina za sitiari na maudhui yake katika vitendawili vya jamii teule.

### **1.7.3 Yaliyoandikwa kuhusu sitiari**

Nzookwa (2011) anaeleza kuwa fasili ya sitiari ni tata na kwa muda mrefu imekuwa fumbo kwa wanaisimu. Wataalam wa isimu waliotangulia walifasili sitiari kama matumizi ya maneno ya lugha, kuwachezea watu shere. Robert (1970), anasema sitiari ni matumizi ya neno potovu linalotumiwa kulinganisha na kuhusisha vitu vilivyo tofauti kitabia na kimaumbile na maana asilia ya neno hilo. Richard (1965), anafafanua sitiari kama ufafanuzi wa jambo fulani kwa kutumia yaliyomo katika jambo hilo, kwamba ni ulinganishi wa vitu viwili bila kutumia neno kama. Kwa hivyo dhana ya sitiari ni uwakilishi na ulinganishi katika matumizi ya ishara na misemo ya kitamathali. Ni kawaida vitendawili kutamkwa kwa kutumia lugha ya mafumbo yenye sitiari, kwa hivyo kuna ulinganishi mkubwa kati ya vitendawili na matumizi ya sitiari kwa sababu vitendawili vingi hubeba sitiari. Vitendawili

venye sitiari huwa na nyuso mbili; uso mmoja ni ule wenye maana iliyo wazi na mwingine ni wa maana fiche. Maana isiyokuwa wazi aghalabu hujificha kwenye sitiari ya kitendawili na hiyo maana ndiyo yenye umuhimu zaidi.

Ufafanuzi wa Richard (1965), ni dhahiri kuliko wa wataalam wengine kwa sababu unaonyesha mlingano na fafanuzi zinazozungumzia kuhamisha maana kutoka muktadha mmoja hadi mwingine. Uhamishaji wa maana unatokana na uwezo wa msemaji wa kulinganisha mambo tofauti tofauti maishani. Waaidha sitiari ni matumizi ya neno la kutoa wasifu wa kitu au mtu fulani kama kitu kingine ili kuonyesha kwamba vyote vina sifa sawa na kufanya ufafanuzi kuwa thabiti zaidi. Mara nyingi sitiari hizo hujenga picha za kitu, mtu, wazo, dhana au maumbile fulani.

Wataalam na watafiti mbalimbali wameshughulikia sitiari, kwa mfano Whigham (2006), ameandika kuhusu umuhimu wa sitiari katika kuondoa wasiwasi. Maelezo yake yamejikita kwenye maoni kuwa ni vigumu mtu kueleza tukio baya kwa maneno ya kawaida. Kwa ajili hiyo, sitiari zinaweza kutumiwa kufafanua mambo hayo magumu katika jamii. Maelezo hayo yalimfaa mtafiti kupambanua maudhui katika vitendawili vya jamii lengwa, tofauti na utafiti huu ni kwamba utafiti huu ulihusu kubaini sitiari katika vitendawili kisha kutoa umuhimu wake kwa kurejelea jamii za Waswahili na Abanyala.

Nyanchama (2004), alihakiki matumizi ya taswira na ishara katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* ili kuona jinsi Abdalatif alivyotumia taswira na ishara katika kuwasilisha maudhui yake. Aliangazia zaidi aina za taswira na ishara zilizotumiwa na jinsi mtunzi alivyozitumia taswira na ishara kuwasilisha maudhui ya diwani hiyo. Alitambua kuwa muktadha wa utunzi, hali ya kisiasa nchini, utamaduni wa Waswahili, tajiriba ya mtunzi ndani na nje ya jela, utamaduni

wake ni baadhi ya mambo yaliyochangia matumizi ya taswira na ishara hizo. Hali hii ilimpa mtafiti fursa ya kuweza kutazama sitiari katika vitendawili vya jamii ya Abanyala kwa kuvilinganisha na vya Waswahili.

Ugonjwa wa Ukimwi umekuwa tishio kubwa kwa jamii hali hiyo ilifanya wengi kubuni majina tofauti ili kuurejelea ugonjwa huo. Hii ndio maana Kobia (2008) akafanya utafiti kuhusu sitiari zinazorejelea ugonjwa wa Ukimwi katika jamii ya Abaluyia, anafafanua kwamba ugonjwa huo hausemwi hadharani, ni mwiko. Hali hiyo imefanya Waluyia kubuni sitiari mbalimbali zinazorejelea. Sitiari hizo zinatokana na majina ya ajali, mimea, wanyama na safari. Utafiti huo ulifaa utafiti huu kwa kumwezesha mtafiti kubainisha maudhui katika vitendawili vya jamii lengwa. Jambo linafanya tafiti hizo mbili kuwa tofauti ni kwamba utafiti huu ulilenga sitiari katika vitendawili.

Matumizi ya sitiari ni mapana, sitiari huweza kutumiwa katika miktadha tofauti ikiwa na lengo tofauti. Katika idhaa mbalimbali za redio nchini Kenya matumizi ya sitiari yamekithiri. Hali hiyo ilimpelekea Ndirangu (2011) kuchunguza matumizi ya sitiari katika idhaa za redio za kiasili nchini Kenya. Alieleza jinsi ambavyo idhaa hizo zilitumia sitiari katika mwaka wa 2007 kabla na baada ya vita vya uchaguzi mkuu wa mwaka huo. Alieleza jinsi ambavyo idhaa nyingi zilivyotumia sitiari kuzua uhasama kati ya makabila tofauti nchini. Hata ingawa utafiti huo unahusu sitiari, tofauti ni kwamba utafiti huu ulishughulikia sitiari katika vitendawili ijapokuwa utafiti huo wa Ndirangu (2011) ulimfaa mtafiti kubainisha aina za sitiari zilizo katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili.

Nzookwa (2011), ametafiti kuhusu 'Dokezo za Sitiari katika Methali za Kiswahili na Kiganda.' Alichanganua uteuzi, kazi na hulka za ishara zinazotumiwa wakati wa kutoa

methali yaani wakati wa maongezi ambao ni msingi wa sitiari na maana katika uwanja wa ulimwengu. Vilevile alibainisha sababu za uchaguzi wa ishara moja badala ya nyingine katika kudokeza jambo fulani. Alitambua kuwa maswala ya ndoa, familia, lugha uchumi yanaweza kutumiwa kuchambua methali za Kiswahili na Kiganda. Utafiti huo ulimfaidi mtafiti kubaini sitiari zilizo katika vitindawili vya Abanyala na Waswahili pia ulimsaidia kueleza maudhui katika vitendawili vya jamii lengwa.

Mchango mwingine kuhusu sitiari umetolewa na Ndungo (2006). Alitazama matumizi ya tamathali za usemi katika lugha ya kisiasa ambapo ameeleza kuwa tamathali hutumiwa katika mazingira halisi ya wanajamii, tamathali hizo hubuniwa na kutumiwa katika shughuli za kila siku za maisha ya wanajamii. Amefafanua zaidi kwamba tamathali ni chombo cha kutolea mawazo ya jamii, huibua hisia zao na kukuza ari yao ya kisiasa ambapo wanasiasa huzitumia kufahamisha na kuwaonyesha wananchi namna wanavyoendelea kunyonywa, kunyanyaswa na kuonewa na viongozi. Tamathali ambazo ameziangalia ni mafumbo, methali na tamathali za ufananisho. Sitiari ni kati ya tamathali za ufananisho alizoshughulikia. Ameonyesha jinsi ambavyo wanasiasa wamelinganisha tabia za baadhi ya viongozi na wanyama kama vile ngiri, kinyonga, panya vipofu. Utafiti huu ulimfaa mtafiti kuchunguza maudhuikatika vitendawili vya Abanyala na Waswahili.

Kutokana na tafiti zilizofanywa na maandishi mengine kuhusu vitendawili na sitiari, ni dhahiri kuwa matumizi ya sitiari katika vitendawili hayajashughulikiwa.

## **1.8 MISINGI YA KINADHARIA**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Semiotiki. Semiotiki ni neno lililotoholewa kutoka neno lenye asili ya Kiyunani lenye maana ya uhakiki wa ishara. Hii ni nadharia yenye

historia ndefu, yenye mielekeo ya uchunguzi wa ishara iliyozuka katika karne ya tano wakati wa Hipocrates, (Eschbach, 1983). Kwa kipindi kirefu mtazamo huu haukutiliwa maanani hadi ulipozinduliwa tena na Nietzsche (1883-1892) na hatimaye Freud, Jung na Heidegger, waliuimarisha mtazamo wenyewe kwa kuupa mwelekeo mpya.

Wataalam hawa walichunguza na kutathmini uhusiano uliopo baina ya dhana ya kitu cha kidhahania au cha mguso na alama ya kiisimu na zisizo za kiisimu. Suala la uashiraji kama anavyoeleza Culler (1981) limeanza kuwa muhimu katika uhakiki wa kazi za fasihi katika miaka ya sabini. Kushika kasi kwa nadharia ya semiotiki katika miaka ya 1960-1970 kumeambatanishwa na mwelekeo wa kuuasi na kuuacha umuundo ulioonekana kama uliofungika au usiobadilika Royle, (1995). Nadharia ya semiotiki katika kuangaza swala la uashiraji humulika jinsi kazi hizo zinavyowasiliana na wasomaji. Nadharia hii inajishughulisha na maana za ishara katika kazi za fasihi, (Innis 1985, Wamitila 2003). Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007), nadharia ya Semiotiki inamwezesha binadamu kuona vitu au hali kama ishara zenye maana. Naye Scholes (1974) anaeleza kuwa semiotiki ni nadharia inayoshughulika na ishara na uashiraji (maana zao) katika matini za kifasihi.

Licha ya nadharia ya semiotiki kufaidi na mikabala hiyo, imefaidi pia kutokana na mawazo ya mwanaisimu wa Ki-Swizi Ferdinand de Saussure ambaye aliwekea misingi katika mwaka wa 1906. Kwa mujibu wa Ferdinand de Saussure, lugha ni mfumo wa ishara. Katika muktadha huo, utamaduni wa fasihi ni zao la utamaduni wa jamii na ni sanaa ambayo hutumia ishara teule za lugha.

Nadharia ya semiotiki iliyohusu fasihi iliweza kutumiwa hapo mwanzoni katika miaka ya 1960 ambapo Jacobson aliibua kanuni au vipengele sita vya msingi vilivyohusishwa katika

mawasiliano ya kifasihi. Vipengele hivyo ni kama vile: mtunzi, mpokeaji, muktadha, matini, utanzu na lugha. Kulingana na mhakiki huyo, mtunzi wa fasihi hususa vitendawili huwasilishwa kwa hadhira kupitia kwa matini teule ambazo hujibainisha katika tamathali za usemi. Kwa kuzingatia utungo wa vitendawili, ilibainishwa kwamba, miundo ya lugha ambayo hutumika zaidi katika uwasilishaji wa utungo huwa ni ya kitamathali. Kadhalika tamathali hizo huweza kuwa za aina mbili: kauli za kitaashira (metonomia) na kauli za kisitiari (kimafumbo).

Kulingana na ufafanuzi huo, lugha ya kitamathali na hasa ile ya kisitiari inapotumiwa katika utunzi wa vitendawili, huukoleza zaidi ujumbe ambao huwasilishwa kwa kujenga mazingira ya usaili na utafakari katika akili ya hadhira, Maitaria (2012).

Aina nyingine ya ubadilishaji wa maneno ni ule wa kisitiari ambapo kimatumizi kauli au maneno hupewa sura mpya. Kulingana na Jacobson, ubadilishaji huo utokeapo katika uwasilishaji wa vitendawili, lugha hiyo huwa ni ya mshindo, kuvutia kutafakarisha na kuliathiri sikio la hadhira. Kwa njia hiyo, ujumbe ambao huwasilishwa huwa si wa moja kwa moja bali ni wa kisitiari au kimafumbo.

Kilichosisitizwa hapa ni kuwa lugha ya kisitiari ni muhimu zaidi na hutumiwa kwa makusudi katika uwasilishaji wa tanzu mbalimbali za fasihi kama vile vitendawili kwa sababu matumizi hayo humtosa msomaji au msikilizaji katika utafakari ili kuweza kuupata ujumbe ambao umewasilishwa kwa njia ya utata na kimafumbo. Kulingana na Wafula (1994) kuwepo kwa sanaa ya fasihi ni thibitisho kuwa matumizi ya kauli za lugha huweza kufinyangwa upya au kiumbuji kwa kuzingatia mitindo ya kitamathali kuwasilishia ujumbe ambao umekusudiwa.


Kadhalika vitendawili huwa vimeundwa kiustadi kwa maneno machache lakini ufafanuzi wake ni mpana kulingana na miktadha ya kimatumizi katika jamii. Kwa hivyo watunzi wana hiari ya kutumia idadi chache ya maneno ili kubainishia au kuwasilishia maana pana. Zaidi ya hayo, imekaririwa kwamba matumizi ya vitendawili au lugha ya kitamathali inapotumika katika utanzu wowote wa fasihi hudhihirika na kufasirika vyema kwa kuzingatia miktadha mahsusi ya mawasiliano na utamaduni wa jamii.

Baada ya kifo cha Ferdinand de Saussure katika mwaka wa 1913, wanafunzi wake: Charlis Bally na Albert Sechehaye waliyaweka mawazo yake pamoja na wakayachapisha katika kitabu kilichoitwa *Course in General Linguistics* katika mwaka wa 1916.

Baadaye nadharia hii iliendelezwa na mwanafalsafa wa Kimarekani Charles Pierce (1977) na mhakiki Barthes (1977) ambao walikuwa na mtazamo tofauti na Saussure. Mtazamo wa kisemiotiki uliohusiana na Ferdinand de Saussure ulijikita katika maana iliyo dhahiri au maana msingi ya ishara bila kuangalia maana batini ya ishara husika. Wataalam hawa walihusisha ishara na maana msingi na pia maana batini kwa kuegemea mantiki. Utafiti huu ulizingatia mtazamo wa C.R. Pierce 1977 ambao pia uliendelezwa na Barthes 1977.

### **Muundo wa nadharia ya semiotiki**

Nadharia hii imeundwa kwa ishara tatu ambazo ni ishara, kiashiria, kiashiriwa zinazohusiana na kuchangiana kama inavyofafanuliwa na Pierce (1977). Mhakiki Pierce aliziweka ishara hizo katika mchoro kama ufuatao:



Mfumo huo wa ishara uliongoza utafiti kama ifuatavyo: ishara ni dhana yenye kuwakilisha au kuashiria kitu fulani. Kiashiria ni wazo au picha inayojengeka katika akili ya msikilizaji kutegemea utamaduni maalum kuhusu jina fulani analolisikia ama misingi ambako ishara inategemezwa ili kufasiriwa kwake kuwezekane. Kiashiriwa ni dhana inayorejelewa katika uhalisi na utamaduni wa jamii maalum.

Utafiti huu ulizingatia mtazamo wa Pierce ambao ulimwezesha kushughulikiwa kwa ishara hususan ishara picha, ishara kamili (elekezi), taashira na ishara tanakali. Ishara kamili ni ishara ya kifonetiki, ishara hii haina uhusiano wa moja kwa moja na neno linaloiwakilisha. Maana zao hutokana na mazoea ya jamii pamoja na utamaduni wa jamii husika. Kwa mfano neno paka ni ishara kwa sababu umbo lake la kifonetiki yaani p-a-k-a halina uhusiano wa asilia na kiashiriwa yaani paka (mnyama) mwenyewe kama anavyokiri Saussure (1974).

Senkoro (1982) anaeleza taashira kwamba ni tamathali ya usemi ambayo hutumia sehemu ya kitu kuwakilisha kitu kizima. Katika aina hii ya tamathali, jina la sehemu ya kitu kimoja au la kitu kidogo kinachohusiana na kingine kikubwa hutumiwa kuwakilisha kitu kamili. Sehemu hii ilimsaidia mtafiti kubainisha umuhimu wa sitiari zilizo katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili.

Mhakiki Barthes (1977) aliiwekea nadharia hii msingi kwa kuzua dhana ya msimbo ili kupendekeza jinsi bora ya kuisoma kazi ya fasihi. Kwa mujibu wa mawazo yake, kila leksia

hudhihirisha msimbo au kaida fulani ambazo huwa muhimu katika kuifasiri. Barthes alizitambua aina tano kuu za misimbo ambazo ni nguzo muhimu katika nadharia ya semiotiki. Nguzo hizo zilimwezesha mtafiti kufasiri sitiari zilizo katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili, umuhimu wa sitiari hizo, vilevile alizitumia kuchunguza sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasilano yao. Nguzo hizo ni:

(i) Msimbo wa matukio

(ii) Msimbo wa kihemenitiki

(iii) Msimbo wa kiseme

(iv) Msimbo wa kiishara

(v) Msimbo wa kirejelezi

**(i) Msimbo wa matukio**

Tukio ni jambo lililofanyika au lililotokea. Msimbo huu unahusu jinsi matukio yanayopatikana katika kazi fulani yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyounda na kuuelewa msuko wa kazi hiyo kwa kuangalia jinsi matukio hayo yanafuatana ki-athari ama kinasibishi. Msimbo huu ulimfaa mtafiti katika kuhakiki matukio ya kiutamaduni katika jamii ya Abanyala na Waswahili yaliyozua baadhi ya sitiari zilizo katika vitendawili vya jamii lengwa.

**(ii) Msimbo wa kihemenitiki**

Msimbo huo unaihusu taharuki, ni msimbo wa kusimulia au kutamba hadithi ambapo unaweza kufumbatwa kwenye anwani ya kazi ya kifasihi. Msimbo huo ulimsaidia mtafiti

kuchunguza sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao.

### **(iii) Msimbo wa kiseme**

Neno seme hutumiwa kuelezea sifa bainifu za kisemantiki. Sifa hizi hutuwezesha kupata picha fulani. Msimbo huu unahusiana na jinsi msomaji atakavyoishia kupata picha katika kazi fulani za kifasihi kwa kuibua fahiwa za maana. Msimbo huu ulimwezesha mtafiti kufafanua picha za maana za sitiari zilizo katika vitendawili zinazojengeka katika akili za watu kutegemea utamaduni wa Abanyala na Waswahili.

### **(iv) Msimbo wa ki-ishara**

Msimbo huu unahusishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanavumbua maana za kiishara katika kazi za fasihi. Ishara huwakilisha viashiriwa fulani, uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni. Msimbo huu ulimwezesha mtafiti kubainisha aina za sitiari zilizo katika vitendawili vya jamii lengwa.

### **(v) Msimbo wa kirejelezi**

Msimbo huu unajengwa kutokana na viashirii vya utamaduni unaorejelewa na tajriba ya maisha. Urejelezi huu huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo kuipa kazi fulani nguzo za kitamaduni. Ndiyo maana kiashirii huweza kuwa kilekile bali kinachorejelewa kikawa tofauti kwa mujibu wa utamaduni na tajriba ya maisha. Msimbo huu ulimsaidia mtafiti kubainisha maudhui katika vitendawili vya jamii ya Abanyala na Waswahili.

Utafiti ulifuata mihimili hiyo ili kubainisha sitiari zilizo katika vitendawili vya jamii ya Abanyala na Waswahili, kwa mihimili hiyo, mtafiti aliweza kubainisha maudhui katika vitendawili vya jamii zinazohusika. Pia aliweza kueleza sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao.

### **1.9 Mbinu za utafiti**

Utafiti ulifanyiwa nyanjani na maktabani. Muundo wa utafiti ulikuwa wa uchunguzi kifani ambapo kikundi maalum cha jamii kama vile familia au jamii nzima huzingatiwa (Kasomo 2006). Muundo huo hulenga utafiti wa kina badala ya upana. Aina hiyo ya utafiti hujumuisha mambo yafuatayo: mtafiti huchukua kitengo kimoja cha kijamii au vingi vya aina hiyo ilmradi wawe na sifa zinazofanana. Kitengo hicho huchunguzwa kwa kina na kwa muda ili kuelewa historia yake. Kitengo kilichoteuliwa huwa kiwakilishi cha jamii nzima na changamano; Mugenda na Mugenda (1999).

Utafiti huu ulianza maktabani kwa kusoma majarida, vitabu, machapisho mbalimbali na tasnifu zinazohusu vitendawili na sitiari. Huko mtafiti alipata maelezo kuhusu vitendawili, sitiari na historia ya jamii ambamo utafiti wake ulijikita. Baada ya kujiandaa maktabani, mtafiti alielekea nyanjani, jamii ambamo utafiti huo ulijikita hasa ni jamii ya Abanyala wapatikanao jimbo la Kakamega, kata ya Navakholo na Waswahili wa Mombasa Mji wKale. Nyanjani, sampuli iliteuliwa kwa mfumo wa mtabakisho kwa kuwachagua shaibu watano, ajuza watano wenye umri wa miaka kati ya sitini na mitano na themanini. Watoto watano wa shule za msingi, hasa wa darasa la sita katika shule tano tofauti waliteuliwa katika maeneo yaliyotengwa. Mtafiti alitumia mbinu kadha za ukusanyaji wa data; hojaji, uchunguzi ushiriki na mahojiano (Mugenda 1999).

Hojaji ni orodha ya maswali yaliyotayarishwa na mtafiti ambapo wajibu wanahitajika kuyajibu. Hojaji wazi ilitumiwa kwa wazee, ajuza na watoto. Vilevile uchunguzi ushiriki ulitumiwa, Kombo na Tromp (2006) wanaeleza uchunguzi ushiriki kuwa ni mbinu ambayo inahusisha utafiti wa data unaohusisha mshirikishi pekee bila kutumia mchunguzwa. Mchunguzi hauliziulizi maswali, yeye hujionea tu. Mbinu hiyo ilifaa zaidi kwa watoto. Mahojiano ni njia ambayo inamruhusu mtafiti kuuliza wajibu wake maswali ana kwa ana. Mbinu hiyo humhitaji mtafiti kuwa na mlahaka mwema na wajibu wake. Mtafiti alitumia njia hiyo akiongozwa na maswali ya mahojiano kwa wajibu ambao hawakuwa tayari kujibu hojaji akizingatia malengo ya utafiti (Mugenda na Mugenda, 1999).

### **1.9.1 Sampuli lengwa**

Sampuli lengwa katika utafiti huu ni shaibu, ajuza na watoto. Uteuzi wa sampuli ulifanywa kimaksudi ili kukusanya data. Kwa ajili hiyo wanafunzi watano watano kutoka shule za msingi tofauti tofauti walitumiwa, darasa la sita ndilo lililolengwa kwa sababu wamekomaa na wanaweza kuainisha vitendawili kulingana na mada mbalimbali. Shaibu na ajuza waliteuliwa kwa misingi ya tajriba na maarifa ya jamii ili kumwezesha mtafiti kutekeleza utafiti huu katika muda ufaao. Ili kufikia idadi kamili ya walengwa, mtafiti aliteua sampuli kwa kutumia mfumo wa mtabakisho.

### **1.9.2 Njia na vifaa**

Mtafiti alitumia njia kadha katika utafiti wake. Alisoma kwa kina maktabani maelezo kuhusu vitendawili, sitiari na maelezo kuhusu jamii ambamo utafiti wake ulitekelezwa na maelezo mengine kwa ujumla kuhusu mada.

Nyanjani mtafiti alitumia mbinu ya hojaji kwa wale wanaojua kusoma na kuandika, pia mahojiano na mjadala ni mbinu zilizotumiwa kwa shaibu na ajuza ambao walipatikana katika vikao mbalimbali vya wazee wa vijiji na chifu akiongozwa na maswali ya utafiti. Katika shule za msingi, mtafiti alitumia mbinu ya hojaji, uchunguzi ushiriki akisaidiwa na walimu wawili wa shule lengwa. Vifaa vilikavyotumiwa katika utafiti huo ni pamoja na maswali ya mahojiano, tepurekoda, video, kalamu na madaftari.

### **1.9.3 Uchanganuzi wa data**

Data ya mahojiano ilipangwa kwa misingi ya sitiari fiche, sitiari kale na sitiari shehenezi. Mtafiti alitumia maelezo ya kina katika uchanganuzi wake wa data huku akizingatia vipengele vifuatavyo: maswali na malengo ya utafiti ambayo ni: kubaini sitiari zilizo katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili, umuhimu wa sitiari katika vitendawili vya jamii lengwa, kwa nini Abanyala na Waswahili hutumia vitendawili katika mawasiliano yao. Mihimili ya nadharia ya semiotiki ilitiliwa maanani ili kuongoza mtafiti kupata aina ya data ambayo inahitajika.

### **1.9.4 Uwasilishaji wa data**

Data iliwasilishwa kwa njia ya kinathari katika sura tano. Sura ya kwanza inahusu utangulizi, mapitio ya maandishi, ya pili inahusu aina za sitiari zinazobainika katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili, ya tatu inahusu maudhui katika vitendawili vya jamii hizo. Sura ya nne inahusu sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao. Sura ya tano inahusu matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo.

## SURA YA PILI

### AINA ZA SITIARI ZINAZOBAINIKA KATIKA VITENDAWILI VYA ABANYALA NA WASWAHILI

#### 2.0 UTANGULIZI

Khatib (1999) anasema kwamba, sitiari ni matumizi ya neno kutoa wasifu wa kitu au mtu fulani kama kitu kingine ili kuonyesha kwamba vyote vina sifa sawa na kufanya ufafanuzi kuwa thabiti. Hali hiyo hutokea kitu kinapopewa jina la kitu kingine. Uhamishaji huu unahusu kutoka kwenye aina moja ya vitu kwenda kwa aina nyingine. Vilevile uhamishaji huo unaweza kutokea kwa mujibu wa kufanana kwa vitu hivyo. Uhamishaji wa maana unatokana na uwezo wa msemaji wa kulinganisha mambo tofauti tofauti maishani. Sura hii imeshughulikia aina za sitiari zinazobainika katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Sitiari ni msingi wa kufichwa kwa maana ambayo msikilizaji au anayetegewa kitendawili anapaswa kukitegua. Sura hii itaelezwa kwa kuzingatia mhimili wa nadharia ya semiotiki inayoeleza kwamba ishara huwakilisha viashiriwa fulani, uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni. Kama ilivyobainika katika sura hii, jamii za Abanyala na Waswahili hutumia ishara tofauti tofauti na matumizi hayo huwa chimbuko la kubuni vitendawili. Baadhi ya sitiari ambazo zilishughulikiwa ni kama vile: sitiarifiche, sitiari shehenezi, sitiari tashhisi, sitiari dhanifu, sitiari changanyi, sitiari changamano na sitiari thabiti.

## 2.1 SITIARIFICHE

Msokile (1993) anafafanua sitiarifiche kama tamathali ya usemi inayolinganisha vitu viwili kwa uhusiano wa mbali, ambapo wazo linalojitokeza huwa mbali kwa kawaida. Kwa mfano kitendawili cha (1) kifuatacho kutoka jamii ya Abanyala kilidhihirika kuwa na sitiarifiche;

### **Kitendawili (1)**

**Abanyala:** *Kuka kemire nokhugulu khulala – olwoba.*

**Tafsiri yake:** Babu amesimama kwa mguu mmoja – uyoga.

Jibu la kitendawili hicho ambacho ni uyoga, limelinganishwa na babu, uhusiano kati ya maneno hayo “babu” na “uyoga” ni wa mbali mno kwa sababu kwa kawaida, babu hawezi kusimama kwa mguu mmoja ingawaje ishara hizi zinafungamana na mazingira ambamo vitendawili hivyo vinachimbuka ambapo urejelezi huo huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo kuvipa vitendawili hivyo nguzo za kitamaduni kama unavyoeleza mhimili wa nadharia ya semiotiki (Innis, 1985). Jambo lilo hilo lilijitokeza katika kitendawili cha (2) kifuatacho cha Waswahili:

### **Kitendawili (2)**

**Waswahili:** Rafiki yangu ana mguu mmoja – uyoga.

Waswahili waliulinganisha uyoga na rafiki, uhusiano huo sio wa moja kwa moja kwani hapa kinachoonyeshwa ni rafiki na kinachorejelewa ni uyoga. Ndiposa mhimili wa nadharia inayoongoza utafiti huu unaeleza kuwa ishara huwakilisha viashiriwa fulani na uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni.

Sitiarifiche vilevile ilibainika katika kitendawili (3) kifuatacho cha Abanyala:

### **Kitendawili (3)**

**Abanyala:** *Endi nabana bange nesiusecha wachia ta – enjukhi.*

**Tafsiri yake:** Nina watoto wangu huwezi kunivamia ukaenda tu- Nyuki.

Watoto katika kitendawili hicho wametumiwa kuficha wazo la nyuki ambao aghalabu ukiwakaribia au ukiuvamia mzinga wa nyuki, nyuki akiwa mmoja huwa tayari kukuvamia. Nyuki wana uhusiano wa karibu na hujitambulisha kama jamii moja kwa hivyo ukivamia mmoja, wote hutetea kwa kumpiga adui. Vile vile wazazi na watoto wanatarajiwa kuwa na uhusiano wa karibu hivyo basi watoto watawatetea wazazi wao hali ya hatari inapotokea ndiposa methali ikasisitiza kwamba “Mkataa uzazi ni mchawi” kwa sababu kizazi kina umuhimu mkubwa katika jamii. Hali iyo hiyo ilidhihirika vilevile katika vitendawili vya Waswahili kupitia kwa mfano wa (4) ufuatao:-

### **Kitendawili (4)**

**Waswahili:** Nilikwenda huko nikaonjeshwa mchuzi – nyigu.

Uvi au nyigu ni mdudu wa jamii ya nyuki mwenye kiuno chembamba anayejenga tumba na anauma sana. Uvi hupenda kujenga mafichoni, mtu anapopita karibu na nyumba yao hushtuka ameshaumwa na uvi. Kwa kawaida, mchuzi wanaonjeshwa watu huwa mtamu tofauti na kitendawili hicho ni kwamba wazo linalojitokeza ni kuumwa na mavu na kuumwa huko huwa ni uchungu mno. Ulinganisho huo wa mchuzi na nyigu ni wa mbali, isitoshe wazo lake li mbali na kile kinachosemwa ila neno hilo ‘mchuzi’ limezoeleka kimatumizi na namna ambavyo nyigu huuma, ni kama kuonjeshwa ‘mchuzi’. Ndiposa mhimili wa nadharia ya

semiotiki ukaeleza kuwa urejelezi huu huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo kukipa kitendawili hicho nguzo za kitamaduni. Hiyo ndiyo maana ya kiashirii kuweza kuwa kilekile bali kinachorejelewa kikawa tofauti kwa mujibu wa utamaduni na tajriba ya maisha.

Vitendawili vya (5) vifuatavyo pia vilionyesha kuwa sitiarifiche imetawala katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili:-

### **Vitendawili (5)**

**Abanyala:** *Endi nomukoye omuleyi sikunyala okhuwoya ekhwi ta - engira.*

**Tafsiri yake:** Nina kamba yangu ndefu haiwezi kufunga kuni – barabara.

**Waswahili:** Kamba yangu ndefu lakini haiwezi kufunga kuni - barabara.

Neno “kamba” katika vitendawili vya jamii hizi za Abanyala na Waswahili limetumiwa kurejelea barabara ambapo hiyo kamba ni ndefu na haiwezi kutumiwa kufunga kuni. Uhusiano huo ni wa mbali kwa misingi ya umbo na matumizi ya kamba.

Katika jamii za Waswahili na Abanyala, ilibainika kwamba mdudu aina ya chawa anaweza kulinganishwa na vitu tofauti; Abanyala wamemlinganisha chawa na aina ya ndege ambaye huishi mwituni ilhali Waswahili wamemlinganisha mdudu yuyo huyo chawa na Bimkubwa aliye ndani ya nywele. Isitoshe Abanyala wamelinganisha msitu na nywele. Hali hiyo imetokea kwa sababu chawa hupenda kujificha, kwa hivyo ulinganisho wa ndege na Bimkubwa kama chawa ni sitiarifiche kwa sababu mawazo yanayorejelewa katika vitendawili hivyo, hayahusiani kwa karibu na jibu la vitendawili hivyo. Vitendawili vya (6) vinaonyesha mifano hiyo:

## **Vitendwili vya (6)**

**Abanyala:** *Esichwinji musichakha - enda mufwiri / enda mu nguo.*

**Tafsiri yake:** Ndege mwituni- chawa ndani ya nywele au nguo.

**Waswahili:** Bimkubwa yumo nyweleni – Chawa.

Chawa ni aina ya mdudu mdogo anayekaa mwilini kwa binadamu au kwenye nguo chafu na hunyonya damu na Bimkubwa ni jina la heshima kwa mama mzazi.

Mifano mingine ya vitendawili vya (7) vya Abanyala na Waswahili vilivyoonyesha sitiarifiche ni kama ifuatayo:

## **Vitendawili vya (7)**

**Abanyala:** *Yema eyi nase neme eyi khukhupe okusacha kuno - Owusuma.*

**Tafsiri yake:** Simama huko nami nisimame huku tupige bwana huyu- Ugali.

**Waswahili:** Kaa huko nami nikae huku tupande mlima - Ugali.

Jinsi ilivyobainika katika vitendawili vya jamii hizi, ugali umelinganishwa na “bwana” katika jamii ya Abanyala na “mlima” katika jamii ya Waswahili. Hata hivyo jambo linalosisitizwa hapa ni kule kukaa pamoja wakati ugali unapoliwa ambapo uhusiano kati ya bwana, mlima na ugali ni wa mbali. Kutokana na mifano hiyo ni bayana kuwa sitiarifiche zi katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili.

## 2.2 SITIARI SHEHENEZI

Msokile (1993) anafafanua sitiari shehenezi kuwa ni sitiari inayoongoza maana na sifa za neno linalolinganishwa kutokana na idadi nyingi ya sifa zilizo katika neno ambalo linalinganishwa. Kama unavyoeleza mhimili wa nadharia inayoongoza utafiti huu, sifa za kisemantiki humwezesha mhakiki kupata picha fulani katika kazi za fasihi kwa kuibua fahiwa za maana; sifa hizo ndizo zinazomwongoza aliyetegewa kitendawili chenye sitiari za aina hii ili aweze kulifikia jibu. Kutokana na utafiti uliyofanywa, aina hii ya sitiari ilibainika katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Kwa mfano:-

### Vitendawili (8)

**Abanyala:** *Chira eyi nase enjire eyi khukutane emberi – omusipi*

**Tafsiri yake:** Pitia huku nami nipitie huku tukutane mbele- mshipi

**Waswahili:** Pitia huku nami nipitie huku, lakini tukutane mbele – mkanda

Ile hali ya kupitisha sehemu moja ya mkanda ama mshipi upande mmoja na nyingine upande wa pili zikakutana katikati, zinamwongoza anayetegewa kitendawili hicho na papo hapo akafahamu kile kinachorejelewa.

Vile vile sitiari shehenezi ilibainika katika vitendawili vya jamii ya Abanyala na Waswahili kupitia kwa vitendawili vilivyotambua sifa ya taa na utambi wake kumaliza mafuta. Sifa hiyo inaongoza hadhira kwa jibu kwani katika jamii ya Waswahili, kitendawili hicho kimetaja nyoka muwi aliye katika kisima cha Zubedah ilhali kitendawili cha Abanyala kimetaja shetani anayekunywa maji kila siku nyumbani. Jambo linaloelezwa waziwazi ni kile kitu kinacholeta hasara mara nyingi nyumbani. Vitendawili vya (9) vinavyofuata, vinaonyesha maelezo hayo:

### **Vitendawili (9)**

**Abanyala:** *Munyumba mwange khuli nesisieno sinywanga amachi wuli nyanga - olutambi lwe taya.*

**Tafsiri yake:** Nyumbani mwangu mna shetani anayekunywa maji kila siku- utambi wa taa.

**Waswahili:** Kisima cha bi. Zubedah kina nyoka muwi ndiye fisadi wa maji- taa na utambi

Vitendawili (10) vifuatavyo vilionyesha wazi kuwa sitiari shehenezi zi katika vitendawili vya jamii zilizoshughulikiwa:-

### **Vitendawili (10)**

**Abanyala:** *Endi na abana bange batachu mulala nachulakho sibakhola emirimo tawe – amaika.*

**Tafsiri yake:** Nina watoto wangu watatu mmoja akitoka hawafanyi kazi – meko.

**Waswahili:** Watoto watatu, akiondoka mmoja kazi haifanyiki – meko

**Waswahili:** Nina bibi watatu, akiondoka mmoja wawili hawafanyi kazi – meko

Lile wazo linalomwongoza anayetegewa vitendawili hivyo ni kwamba figa moja tu likiondolewa ni vigumu kwa chungu kuweza kuinjikika vyema. Kwa hivyo, mfano huo ni wa sitiari shehenezi kwa sababu maelezo ya kule kushirikiana kwa mafiga matatu kama watoto au bibi, mmoja wao akiondoka kazi haiwezi kuendelea kama kawaida. Kama unavyoshikilia mhimili wa nadharia ya semiotiki, urejelezi kama huo huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo kuvipa vitendawili

hivyo nguzo za kitamaduni. Ndio maana kiashirii huweza kuwa kile kile bali kinachorejelewa kikawa tofauti kwa mujibu wa utamaduni na tajriba ya maisha.

Swala la nyumba isiyo na mlango lilijitokeza katika aina hii ya sitiari, ilidhihirika kwamba nyumba isiyo na mlango ilifananishwa na yai. Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004), yai ni kitu chenye kaka gumu na ute wa rangi nyeupe na manjano ndani ambacho hutagwa na ndege, kuku au wanyama watambao na husababisha kuzaliwa kiumbe kingine. Mara nyingi yai huwa halina upenu wowote ndio maana hali hiyo inampeleka anayetegewa kujiuliza swali ni nyumba ipi hii isiyo na mlango? Mifano hiyo ni kama ifuatayo ya vitendawili vya (11):

#### **Vitendawili (11)**

**Abanyala:** *Enju yange yiumakho omuliango – ewuyu*

**Tafsiri yake:** Nyumba yangu haina mlango – yai

Mbali na mifano hiyo, sitiari shehenezi ilijidhihirisha katika vitendawili vya (12) vya Abanyala na Waswahili vifuatayo:

#### **Vitendawili (12)**

**Abanyala:** *Enjangiriye naye atong'ire enyuma – engoro*

**Tafsiri yake:** Nimetangulia naye amebaki nyuma - kisogo

**Waswahili:** Naenda na mwenzangu nikigeuka nyuma simuoni – kisogo

Kisogo ni sehemu ya nyuma ya kichwa, unapogeuka huwezi kukiona, mara nyingi mtu anapotembea, kisogo hubaki nyuma. Sifa za kisogo kuwa nyuma kwenye sehemu ya kichwa zinamwongoza anayetegewa kuweza kutambua kwa haraka jibu la kitendawili hicho.

Vitendawili vingine vilivyoonyesha sitiari shehenezi viliegemea upande wa mavazi, maneno kama vile 'kuvaa nguo nyingi au makoti mengi' ni maneno yanayomwelekeza anayetegewa kitendawili kama hicho kutambua kitu kinachokuwa kama nguo au kilichofunikwa kwa wingi hivyo basi ikiwa hindi linapatikana katika jamii yake basi atalitambua mara moja. Kitendawili kama hicho kwa ambavyo kinarejelewa na mhimili wa nadharia ya semiotiki unaohusishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanavumbua maana za kiishara katika kazi za fasihi, ishara hizo huwakilisha viashiriwa fulani na uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni. Vitendawili hivyo ni:-

### **Vitendawili (13)**

*Abanyala: Akhamakoti mangi – etumwa*

**Tafsiri yake:** Mwenye makoti megini – hindi

**Waswahili:** Mke wangu ni mfupi lakini huvaa nguo nyingi – hindi

Ni bayana kuwa sitiari shehenezi imetawala katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili kupitia kwa mifano iliyodondolewa.

### **2.3 SITIARI TASHHISI**

Kulingana na Murdoch (2008), sitiari tashhisi ni sitiari inayolinganisha tabia za watu na vitu visivyo na uhai, kwa mfano ulinganisho wa mto na rafiki, vicheko na mabonde, na ulinganisho wa jinsi mtu anavyoonekana vizuri kunavyozungumzia namna alivyo. Anatoa

mfano kuwa kukumbuka ni sawa na mwanamke mwenda wazimu ambaye huficha matambara na anatupa chakula. Kinachodhihirika katika mifano hiyo ni kwamba baadhi ya tabia za watu zimelinganishwa na vitu visivyo na uhai, ndiposa mhimili wa nadharia inayoongoza utafiti huu ukakiri kwamba ishara huwakilisha viashiriwa fulani na uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni.

Sitiari tashhisi ilibainika katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili, kwa mfano katika jamii ya Waswahili kitendawili kifuatacho cha (14) kinaonyesha matumizi ya sitiari tashhisi:

#### **Kitendawili (14)**

**Waswahili:** Nyanya yako ana huruma kukubeba ulalapo – kitanda

Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004), nyanya ni mama mzaa baba au mama, bibi. Nacho kitanda ni kifaa chenye umbo la mstatili na miguu minne kinachotumiwa kwa kulalia. Kwa hivyo katika kitendawili hicho, kitanda kinaelezwa kwa kutumia sitiari ya kitashhisi hivi kwamba kinalinganishwa na mtu – nyanya aliye na uwezo wa kumtuliza mtu anapokuwa amechoka ama anapokuwa na maumivu.

Sitiari tashhihi pia ilidhihirika katika vitendawili vya Waswahili kupitia kwa mfano ufuatao wa (15):

#### **Kitendawili (15)**

**Waswahili:** Nyanya anaota moto kwa mgongo – uchaga

Uchaga ni kichanja kinachotumiwa kwa kuhifadhia au kuanikia kuni au vitu. Kwa mara nyingi, akina nyanya au mama ndio wanaojihusisha na mambo ya uhifadhi wa kuni isitoshe kuni hizo zinapohifadhiwa, hukauka kwa utaratibu jinsi ambavyo nyanya huwa karibu na

moto na huota kwa utaratibu pia. Hali hiyo iliwafanya Waswahili kuona kuwa kwa vile uchaga wa kuni huwa karibu na sehemu ya kuwashia moto, ndiposa wakahusisha nyanya na uchaga (Kulingana na Mama Fauzia).

Mfano ufuatao wa kitendawili (16) kutoka jamii ya Waswahili vilevile unaonyesha ulinganisho uliotumia sitiari tashhisi:

### **Kitendawili (16)**

**Waswahili:** Wanawake mafundi hawa! Hukandika nyumba kubwa lakini wanakoteka maji hakujulikani – Mchwa wanapojenga kichuguu chao.

Kitendawili hiki kwa ambavyo kinarejelewa na mhimili unaohusishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanavumbua maana za kiishara katika kazi za fasihi, ishara hizo huwakilisha viashiriwa fulani ambapo uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo akilini. Kwa msingi huo, kitendawili hiki kimetumia sitiari tashhisi pale ambapo wadudu ambao ni mchwa wamepewa uwezo wa kukandika vichuguu vikubwa kwa kutumia mate yao jinsi wanavyofanya wanawake. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) inaeleza kukandika kama kubandika udongo ili ushike katika kiambaza, ilitambuliwa kwamba katika jamii ya Waswahili, kazi ya kukandika hufanywa na wanawake hii ni kwa sababu utamaduni wao hauruhusu mwanamme kukandika kwa ajili kazi hiyo inaaminiwa kwamba ni nyepesi mno ikilinganishwa na nguvu walizonazo wanaume (haya nikulingana na Mama Fauzia).

Sitiari tashhisi pia ilitambuliwa katika vitendawili vya Abanyala. Ulinganisho huo ulibainika kupitia kwa mifano ifuatayo ya (17):

### **Kitendawili (17)**

**Abanyala:** *Omukhana kayindula emoni muwenywe omwo aritekha nyinga sina – omukherekha*

**Tafsiri yake:** Msichana mwenye macho makubwa aliye nyumbani mwenu ataolewa lini – chumvi ya kiasili.

Katika kitendawili hicho, msichana amelinganishwa na ‘chumvi ya kiasili’ ya Abanyala. Kulingana na jamii hiyo, majukumu ya msichana yamelinganishwa na kazi ya ‘chumvi’. Kwa kawaida ‘chumvi’ hiyo haiishi katika nyumba za Abanyala ndiyo maana wakaihusisha na msichana ambaye hajaolewa kwani kila uchao msichana huyo hutekeleza majukumu yaliyo nyumbani mwao jinsi chumvi inaavyotumiwa kila mara.

Ulinganisho wa babu na kitunguu katika kitendawili cha Abanyala ni ulinganisho wa sitiari tashhisi, aina hiyo ya sitiari ilibainika kupitia kwa mfano wa (18) ufuatao:

### **Kitendawili (18)**

**Abanyala:** *Kuka kefwalanga amakoti maangi – esitunguyu*

**Tafsiri yake:** Babu huvaa makoti mengi – kitunguu

Koti ni vazi zito linalovaliwa juu ya nguo nacho kitunguu ni mmea ambao shina lake lina tabaka za mviringo lenye mvuke unaomcheza na kuwasha machoni na hutumika kama kiungo katika chakula. Wazee huvalia makoti mengi kwa ajili ya kuzuia baridi; kadri umri unavyosonga, ndivyo kiwango cha kuweza kustahimili baridi kinavyopungua isitoshe wazee wengi huvaa makoti ili kuhifadhi vitu hasa pesa. Hali iyo hiyo imehamishwa hadi kwenye vitunguu vinavyojipanga juu kwa juu.

Mfano wa kitendawili cha (19) kinachofuata kinatambua sitiari tashhisi katika vitendawili vya Abanyala:

### **Kitendawili (19)**

**Abanyala:** *Kukhu atundukira khungira – esa*

**Tafsiri yake:** Nyanya anajikokota njiani – kiwavi

Utafiti huu ulitambua kuwa wengi wa akina nyanya ni wakali sana (Agnes Liaka), kujikokota kwao na ukali wao umelinganishwa na kiwavi – mdudu mwenye miguu mingi ambaye aghalabu huwa na manyoya yanayowasha aliye katika hatua ya pili ya ukuaji wa vipepeo na nondo. Ishara hizo huwakilisha kiashiriwa (kiwavi) ambapo uhusiano kati ya ishara na kiashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni (Pierce, 1977).

Kutokana na mifano hiyo ni bayana kwamba aina ya sitiari tashhisi ilibainika katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili.

## **2.4 SITIARI THABITI**

Aina hii ya sitiari itaelezwa kwa kurejelea mhimili wa nadharia ya semiotiki, mhimili huo hutumiwa kuelezea sifa bainifu za kisemantiki zinazomwezesha mhakiki kupata picha fulani. Mhimili huo unahusiana na jinsi msomaji anavyoishia kupata picha katika kazi za kifasihi kwa kuibua fahiwa za maana. Murdoch (2013) anaeleza sitiari thabiti kama ulinganisho unaotumia kitu thabiti kueleza dhana fulani. Anafafanua zaidi kuwa ni matumizi ya kitu kinachofanana wazo fulani ndicho kinachotumiwa kueleza wazo hilo, kwamba matumizi ya kitu thabiti hueleweka kwa uwazi kuliko kile kinachozungumziwa. Anatoa mfano wa utunzi wa yai kama njia moja ya kuwafunza watu kumakinika, hali kadhalika mwandishi huyu

anaeleza zaidi kwamba matumizi ya vitu thabiti hurahisisha uelewa wa jambo kwa haraka. Hii ni kwa sababu vitu ni halisi kuliko maneno yanayohusu kitu chenyewe vilevile vitu halisi huibua shauku iwapo vitatumiwa kama utangulizi wa wazo linalozungumziwa. Aina hii ya sitiari ilibainika katika baadhi ya vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Kwa mfano kitendawili kifuatacho cha (20) cha Waswahili kinaonyesha ulinganisho wa sitiari thabiti.

### **Kitendawili (20)**

**Waswahili:** Nyumba yangu ndogo imejaa watu – kinywa na meno.

Kitendawili hiki kwa ambavyo kinarejelewa na mhimili unaoeleza kwamba ishara huwakilisha kiashiriwa fulani na uhusiano kati ya ishara na kiashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni, kinywa kimelinganishwa na nyumba. Ishara hiyo, ndiyo inayoibua shauku ya anayetegewa kuweza kufaragha katika mazingira yake na atambue ni nyumba ipi hii iliyojaa watu? Kupitia kwa ulinganisho huo, anayetegewa huvuta nadhari ya jinsi meno yalivyojaa na kujipanga mdomoni na hivyo akatambua kwa haraka jibu la kitendawili hicho.

Mfano wa kitendawili (21) cha jamii ya Waswahili kifuatacho unaonyesha kuwa sitiari thabiti i katika vitendawili vya jamii lengwa:

### **Kitendawili 21**

**Waswahili:** Pango lenye mawe meupe na mkeka mwekundu – mdomo

Katika kitendawili hicho, ishara ya pango kwa maana ya mdomo imejitokeza, vilevile mawe meupe yametumiwa kuashiria meno na mkeka mwekundu ukaashiria ulimi. Kiashirii cha mkeka kimetumiwa kuangaza ule uwezo wa ulimi kukunjika. Mbali na mfano huo, kitendawili (22) kifuatacho kutoka jamii ya Waswahili, umetambua aina ya sitiari thabiti:

## **Kitendawili 22**

**Waswahili:** Zulia langu haliwekwi sakafuni bali ukutani – pazia

Zulia ni mkeka wa manyoya au sufu, katika kitendawili hicho, pazia limelinganishwa na zulia kutokana na upana wake dhana ambayo itabidi anayetegewa awe nayo mawazoni ili aweze kuking'amua kitendawili hicho.

Katika vitendawili vya Abanyala, baadhi ya mifano ifuatayo ilibainisha sitiari thabiti:

## **Kitendawili 23**

**Abanyala:** *Endi nyumba yange yirikho omuriango mulala na madirisia kabiri – esinyasa.*

**Tafsiri yake:** Nina nyumba yangu yenye mlango mmoja na madirisha mawili – kaptula.

Katika mfano huo, nyumba imetumiwa kuashiria kaptula ambayo aghalabu huwa na sehemu yenye kiuno inayoashiriwa na mlango ambao ni uwazi wa kuingilia na kutokea penye uwazi zaidi. Viashirii vya madirisha mawili vimetumiwa kuashiria sehemu inayoingizwa miguu, kama anavyoeleza Innis (1985), urejelezi huo huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji kwa njia hiyo kukipa kitendawili hicho nguzo za kitamaduni.

Sitiari thabiti iliweza kutambulika katika kitendawili (24) kifuatacho cha Abanyala:

## **Kitendawili 24**

**Abanyala:** *Endi akachi wamawa nesikanjomakho ta – olulimi.*

**Tafsiri yake:** Niko katikati ya miiba lakini hainichomi – ulimi

Meno katika kitendawili hicho yamelinganishwa na miiba, miiba hiyo imezunguka ulimi lakini haichomi ulimi huo. Matumizi ya ishara ya miiba kukizunguka kitu fulani (kiashiriwa) humfanya anayetegewa kitendawili hicho kujenga dhana inayohusiana na jibu la kitendawili hicho.

Watoto katika jamii inaaminiwa kuwa wana uhusiano wa karibu na wazazi wao na panapotokea jambo la dharura kuhusu wanajamii au wazazi wao, wao huwa tayari kuwatetea kwa vyovyote vile. Hali hiyo iliwafanya Abanyala kubuni kitendawili chenye uhalisi wa hali hiyo kwa kutumia watoto kama ishara kamili ya nyuki. Kitendawili hicho ni:

### **Kitendawili 25**

**Abanyala:** *Endi nabana bange nesiusecha wachia ta – enjukhi*

**Tafsiri yake:** Nina watoto wangu huwezi kunivamia ukaenda tu.

Mifano hiyo tofauti tofauti iliyotolewa, inaonyesha kuwa sitiari thabiti ni kati ya sitiari zinazobainika katika vitendawili vya jamii ya Abanyala na Waswahili.

## **2.5 SITIARI CHANGANYI**

Sitari changanyi ni matumizi ya sitiari tofauti tofauti zinazopatikana katika usemi mmoja au sentensi moja; Murdoch (2008). Naye Steffies (2013) anafafanua aina hii ya sitiari kama mfuatano wa sitiari zinazokinzana. Baadhi ya vitendawili vya Waswahili vilionyesha kuwa na aina hii ya sitiari, kwa mfano:

## **Kitendawili 26**

**Waswahili:** Damu ya simba imetawanyika lakini nzi hawathubutu kutua wakala ingawa wanaitamani sana – moto.

Kitendawili hiki kinaonyesha jinsi vitendawili vinavyoweza kuchanganya sitiari au kutumia sitiari changanyi. Moto ni muhimu ingawa ni hatari, jambo hilo limelinganishwa na damu ya simba vilevile nzi katika kitendawili hicho wanaweza kusimamia watu wanaofaidika na moto ingawa wanafahamu hatari yake.

Hali kadhalika sitiari ya ‘mwana’ na ‘vyakula’ katika kitendawili (27) kinachofuata, zimetumiwa kurejelea moto ambao una uwezo wa kuchoma na kuteketeza vitu vikavu na kutoa ndimi nyekundu. Ishara hizo mahsusi zimetumiwa ili kuwasilisha ujumbe katika kitendawili hicho kwa kuzingatia utamaduni wa jamii ya Waswahili (Herdley, 1998).

## **Kitendawili 27**

**Waswahili:** Mwanangu hajaota meno; lakini hutafuna vyakula vikavu vikavu kwa kuvilamba na ulimi wake laini – moto.

Mfano mwingine unaoonyesha sitiari changanyi katika vitendawili vya Waswahili umetumia sitiari za mfalme aliyevaa mavazi mekundu na askari wake waliovaa mavazi meupe. Sitiari hizo zimetumiwa kuwakilisha ulimi ulio na rangi ya wekundu ambao ni mfalme na meno ambayo yana rangi nyeupe yanayouzunguka ulimi ambayo ndio askari wanaomchunga mfalme. Kitendawili chenyewe ni:

## Kitendawili 28

**Waswahili:** Mfalme amevaa mavazi mekundu na amezungukwa na askari wenye mavazi meupe – ulimi.

Mifano iliyotolewa katika sehemu hii, inaonyesha waziwazi kwamba sitiari changanyi imetumiwa katika vitendawili vya Waswahili.

### 2.6 SITIARI CHANGAMANO

Ni sitiari ambazo maana ya kawaida huelezwa kupitia kwa sitiari mbalimbali nyepesi (Nordquist, 2013). Sitiari ya aina hii, huchukua sitiari nyepesi na kuongeza kwenye sitiari changamano. Hii ndiyo aina ya sitiari ambayo kwa mara nyingi hutumiwa katika vitendawili kwa sababu baada ya kuchangamana, hukanganya aliyetegewa hivyo ikawa vigumu kwake kupata jibu la kitendawili alichotegewa. Katika usemi wa kawaida, mifano inayotolewa na Nordquist (2013) ni kama ifuatayo: ‘amehisi amechemka’ sitiari hiyo inaonyesha mtu fulani kupandwa na hasira. Katika muktadha huo, kuchemka kunaonyesha kiwango cha ukuwaji wa hasira. Hali kadhalika ‘kuongeza mwanga kwa jambo’ mwanga hapa limetumiwa kuonyesha kuzidisha uelewa wa jambo. Kama unavyoeleza mhimili wa nadharia iliyoongoza utafiti huu, sifa bainifu za kisemantiki hutuwezesha kupata picha fulani za kifasihi kwa kuibua fahiwa za maana. Picha hizo ndizo nguzo zinazomwelekeza aliyetegewa kitendawili fulani kwenye jibu lake.

Kupitia kwa mfano ufuatao wa (29) wa kitendawili cha Waswahili, mbingu na nyota zimeelezwa kupitia kwa sitiari mbalimbali za taa ya Mungu na chawa. Hii ni kwa sababu nyota zilizoko mbinguni mara nyingi huwa nyingi na ni ndogondogo, sifa hizo za kujaa kwa wingi ndizo zinazomwelekeza aliyetegewa kupata jibu la kitendawili hicho.

## Kitendawili 29

**Waswahili:** Taa ya Mungu imejaa chawa kochokocho – mbingu na nyota zake.

Katika kitendawili (30) cha Waswahili, Ukambaa wangu mwekundu una uwambe, ukiudara lazima ujikune – safu ya siafu, kuna sitiari ya ukambaa na uwambe. Ukambaa ni ugwe mnene unaosokotwa kwa muwaa au majani ya tumbaku ilhali uwambe ni kitu kinachowasha, kukanganya kunaongezeka zaidi kwenye kitendawili hicho baada ya neno ‘ukiudara’ linapongezwa kwenye kitendawili hicho. Hata hivyo maana za maneno hayo zinamwelekeza aliyetegewa kitendawili hicho kupata jibu lake na wazo linalojitokeza. Wazo lake kuu ni kujihadhari na jambo la hatari. Vile unavyosema mhimili wa nadharia inayoongoza utafiti huu ni kuwa sifa bainifu za kisemantiki hutuwezesha kupata picha za kifasihi kwa kuibua fahiwa za maana ndivyo aliyetegewa anavyoishia kupata jibu la kitendawili hicho.

### 2.7 SITIARI DHANIFU

Lakoff na Johnson (1980) wanaeleza sitiari dhanifu kama uelewa wa wazo kupitia kwa wazo lingine, kwamba sitiari dhanifu hukuza uwezo wa kuwasiliana na kuwaza, wanaeleza zaidi kuwa matumizi ya lugha ya kila siku yamejaa sitiari dhanifu ambazo hatuzitambui kwa mfano: ‘ubishi ni ghasia’, dhana ya ghasia huturahisishia kuelewa namna ya kukabiliana na ubishi. Sitiari dhanifu hutumia wazo moja kwa kulihusisha na lingine ili kuelewa jambo fulani waziwazi, inaamiwa kuwa uelewa wa sitiari dhanifu husaidia kukumbuka msamiati wa lugha ngeni.

Aina hii ya sitiari ilibainika katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili kupitia kwa mifano ifuatayo ya 31:

### **Kitendawili 31**

**Waswahili:** Anakula chakula cha afya lakini hanoni – sufuria

Sufuria na chakula vimetumiwa kisitiari kuonyesha jinsi ambavyo watu wengi hushiriki katika kutenda jambo na huenda jambo hilo lisiwafaidi. Wazo hilo linatokana na dhana kwamba sufuria hutumiwa kupikia vyakula vya kila aina lakini haishiriki katika ulaji wa vyakula hivyo.

Kama unavyoeleza mhimili wa nadharia inayoongoza utafiti huu sifa bainifu za kisemantiki zinamwezesha msanii kupata picha katika kazi za kifasihi kwa kuibua fahiwa za kimaana, hali hiyo ndiyo inayomwongoza mhakiki kutambua kwamba mauti ndiyo yanayorejelewa katika vitendawili vifuatavyo (32) vya Abanyala na Waswahili:

### **Vitendawili 32**

**Abanyala:** Arianga ne sikekuchanga ta – efwa

**Tafsiri yake:** Anakula lakini hashibi – mauti

**Waswahili:** Anakula lakini hashibi – mauti

Mauti ni kifo au hali inayomfanya binadamu kukosa uhai. Binadamu wamekuwa wakifa tangu zamani na bado wanaendelea kufariki, mauti hayatosheki.

Ulinganisho wa ‘kunywa huku wengine wamesimama’ unaojitokeza katika kitendawili (33) cha Abanyala, unaeleza dhana ya watu wengine katika jamii kutoshirikiana na wenzao ilhali jambo lilo hilo huenda likawafaidi maishani na jamii kwa ujumla.

### **Kitendawili 33**

**Abanyala:** *Kino kinywa ne kino kiemire – enjika chieng'ombe*

**Tafsiri yake:** Hawa wanakunywa na hawa wamesimama – pembe za ng'ombe.

Mifano iliyotolewa kutoka jamii za Waswahili na Abanyala, zinaonyesha bayana kwamba sitiari dhanifu i katika vitendawili vyao.

### **2.8 HITIMISHO**

Sura hii imeshughulikia aina mbalimbali za sitiari zinazobainika katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili, kwa misingi ya nadharia ya semiotiki ni dhahiri kuwa kuna sitiari tofauti tofauti katika vitendawili vya jamii za Abanyala na Waswahili. Baadhi ya sitiari zilizoshughulikiwa ni sitiari fiche, sitiari shehenezi, sitiari tashhisi, sitiari thabiti, sitiari changanyi, sitiari changamano na sitiari dhanifu.

Ilidhihirika wazi kuwa sitiarifiche ni sitiari inayolinganisha vitu viwili kwa uhusiano wa mbali ambapo wazo linalojitokeza huwa mbali kwa kawaida. Baadhi ya vitu au maneno yaliyotumiwa kurejelea sitiarifiche ni kama vile babu, nyuki, watoto, kamba, barabara miongoni mwa majina mengine.

Ilitambuliwa kuwa vitendawili vingi vya Waswahili na Abanyala vilitawaliwa na sitiari shehenezi. Sitiari shehenezi ni sitiari inayoongoza maana na sifa za neno linalolinganishwa, kilichotambuliwa hapa ni kuwa sifa za kile kinacholinganishwa, huongoza anayetegewa kitendawili kisha akaweza kupata jibu la kitendawili hicho. Ndiposa nadharia ya semiotiki ikaeleza kuwa sifa bainifu za kisemantiki hutuwezesha kupata picha fulani katika kazi fulani

za kifasihi kwa kuibua fahiwa za maana. Kutokana na hayo, baadhi ya maelezo ya vitendawili yalielekea kutoa picha za mkanda, meko, mayai, kisogo na hindi.

Fauka ya hayo sitiari tashhisi ilishughulikiwa, aina hii ya sitiari hulinganisha tabia za watu na vitu visivyoonekana ama vitu visivyo na uhai. Kama inavyoshikilia nadharia ya semiotiki, ishara huwakilisha viashiriwa fulani, uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni. Utafiti huu ulitambua vitu mbalimbali ambavyo vililinganishwa na vitu visivyo na uhai kama vile kitanda, uchaga, mchwa, chumvi na kitunguu.

Katika utafiti huu, sitiarifiche, sitiari shehenezi na sitiari tashhisi zilitawala katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Sura inayofuata, utafiti imeshughulikia maudhui katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili.

## SURA YA TATU

### MAUDHUI KATIKA VITENDAWILI VYA ABANYALA NA WASWAHILI

#### 3.0 UTANGULIZI

Sura hii imeshughulikia maudhui katika vitendawili vya jamii za Abanyala na Waswahili. Maudhui haya yameelezwa kwa kuzingatia mhimili wa nadharia inayoongoza utafiti huu unaohusu jinsi matukio yanayopatikana katika simulizi fulani yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyouunda na kuuelewa msuko wa kazi hiyo kwa kuzingatia jinsi matukio hayo yanavyofuatana ki-athari ama kinasibishi. Tukio ni jambo lililofanyika ama lililotokea, kwa kuzingatia mhimili huo, mtafiti aliweza kuhakiki matukio ya kitamaduni katika jamii za Abanyala na Waswahili yaliyozua sitiari zilizoweza kutumiwa katika vitendawili vyao. Ilitambuliwa kwamba sitiari zilizotumiwa zilitokana na matukio mbalimbali yaliyohusu vifo na magonjwa, mifumo ya kihistoria, vyakula, mazingira na mabadiliko ya kiwakati.

#### 3.1 Sitiari kama kiashirii cha magonjwa na kifo

Katika historia ya binadamu, kuna magonjwa mbalimbali yaliyoibuka na kusababisha watu kupoteza maisha. Ukosefu wa tiba pia ulichangia katika vifo hivyo. Lakini kadiri binadamu anavyopiga hatua za kimaendeleo ndivyo akili yake inavyopevuka (Momanyi, 2006). Baadhi ya maradhi yanayoogopewa katika historia ya binadamu ni kama vile kifua kikuu, tauni, ndui, homa ya matumbo, tetemaji, UKIMWI na kipindupindu miongoni mwa mengine. Magonjwa haya, yaliweza kuundiwa sitiari ambazo baadaye zilitumiwa katika vitendawili vya jamii ya Waswahili. Kwa mfano:-

### **Kitendawili (34)**

**Waswahili:** Mgonjwa wa ndui ananing'inia kwenye mti – fenesi / stafeli / nanasi

Katika kitendawili hiki (34), tunda lenye vipete vilivyochongoka limefananishwa na ngozi ya mgonjwa wa ndui mwenye vipete vingi mwilini. Tukio hilo la kuwepo kwa ugonjwa unaosababisha mwili kuwa na vipete vinavyolinganishwa na vipete vya fenesi, limepelekea sitiari tashhisi (mgonjwa wa ndui) kutumiwa ikilinganisha ugonjwa huo na fenesi.

Hivi leo jamii inakabiliwa na ugonjwa hatari wa UKIMWI. Kama anavyodai Kobia (2001), kuzuka kwa ugonjwa huo, kumefanya tafiti mbalimbali za kilugha kufanywa. Kwamba sitiari mbalimbali zinazotaja mambo kama vile: radi, upepo, safari, mamba, funza, jitu, ufagio na sindano miongoni mwa zingine zilibuniwa na jamii ya Abaluyia ili kuurejelea ugonjwa huo, tukio hili limepelekea jamii ya Abanyala kutumia baadhi ya sitiari hizo kuunda vitendawili vinavyolinganishwa na ugonjwa huo. Kwa mfano kitendawili (35) kifuatacho kinaulinganisha ugonjwa huo na zimwi:

### **Kitendawili (35)**

**Abanyala:** *Namunyu kuri erwanyi eyi – owulwaye*

**Tafsiri yake:** Zimwi liko huko nje – ugonjwa

Ngure (2004) anafafanua kuwa mazimwi ni viumbe visivyokuwa binadamu wala wanyama, huwa ni viumbe wa kuogofya, wasiokuwa na huruma na ambao aghalabu huwa ni viwakilishi vya uovu. Jamii za Abanyala na Waswahili zinaamini kwamba mazimwi yalikuwa na uwezo mkubwa na maumbile tofauti tofauti ya kustaajabisha. Watu wengi walitahadharishwa kutembea ovyo ovyo ili wasije wakakumbana na jitu ambalo lingewaangamiza. Hali iyo hiyo

ndiyo iliyolinganishwa na ugonjwa hatari unaowaangamiza watu baada ya kuwa na mienendo isiyofaa.

Dhana kuwa Wazungu ndio walio na akili na busara kushinda binadamu wengine bado inashikiliwa na jamii mbalimbali katika janibu zetu. Mielekeo ya wengi ni kuwa utaalumu wa kisayansi uliasisiwa na wazungu. Aidha mzungu ndiye mvumbuzi wa mizungu na teknolojia zote za kuimarisha na kurefusha maisha. Hata hivyo mzungu ameshindwa kuasisi mbinu za kuzuia kifo kutokea. Kutokana na tukio hili, vitendawili vyenye sitiari ya kifo kuwashinda wengi hata mzungu, vilibuniwa.

Waswahili waliweza kubuni kitendawili kifuatacho (36) chenye ujumbe uo huo, kwamba hamna kiumbe anayeweza kukikwepa kifo ndiposa wakalinganisha kifo na kitu chenye nguvu zaidi hata mzungu hawezi kukizuia kinapofika. Kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki, urejelezi huo huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo kukipa kitendawili hicho nguzo za kitamaduni. Urejelezi huo hujengwa kutokana na viashirii vya utamaduni na tajriba ya maisha. Kwa sababu hiyo Waswahili walichagua neno 'mzungu' kuonyesha mtu mwenye uwezo mkubwa, kinaya ni kwamba kifo kimemshinda anayedaiwa kuwa na uwezo huo mkubwa.

### **Kitendawili (36)**

**Waswahili:** Hata Mzungu ameshindwa – kifo

Licha ya sitiari kuonyesha kwamba vifo vimewashinda wengi, sitiari zingine zilitumiwa kuonyesha kuwa baada ya kifo, hakuna kurudi. Kwa kawaida jani la mti likianguka haliwezi kurudi mtini, huo huwa mwisho wake vivyo hivyo mtu afapo, hawezi kurudi. Hali hiyo ndiyo inayojidhihirisha katika vitendawili (37) vifuatavyo vya Abanyala na Waswahili:

### **Vitendawili (37)**

**Abanyala:** *Kukhu nawuya awuyiranga elala – esafu*

**Tafsiri yake:** Nyanya akihama, huhama kabisa – tawi

**Waswahili:** Akiondoka hawezi kurudi – jani la mti

Kutokana na mifano mbalimbali iliyotolewa ni dhahiri kuwa sitiari katika vitendawili vya jamii za Abanyala na Waswahili hutumiwa kuashiria magonjwa na kifo.

### **3.2 Sitiari kama kiashirii cha kuwepo kwa mifumo ya kihistoria iliyoshuhudia majilio ya wageni.**

Kung'ang'aniwa kwa bara Afrika na mataifa mengi yaliyoendelea, kulisababisha wageni mbalimbali kukimbilia Mwambao wa Pwani ya Kenya. Wageni hao walikuwa Wareno, Waholanzi, Wazungu, Wafaransa, Waarabu, Waajemi na Wagriki, majilio ya wageni hao yalishuhudiwa na kuletwa kwa vitu mbalimbali kwa mfano silaha (bunduki), vioo, divai, kauri, hariri, vyombo vya nyumbani miongoni mwa vingine (Ochieng, 1985). Baadhi ya vyombo hivyo vilisababisha kuundwa kwa sitiari mbalimbali zilizolinganishwa navyo ndiposa mhimili wa nadharia inayoongoza utafiti huu ukaeleza kuwa ishara huwakilisha viashiriwa fulani. Uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni kwa hivyo, ishara ya 'mlango wa chuma' katika kitendawili cha (38), imetumiwa kuwakilisha bunduki, dhana ambayo i mawazoni mwa wanajamii na mlango huo unapofunguliwa, maafa hutokea.

### **Kitendawili (38)**

**Waswahili:** *Tamu taaluma, mlango wa chuma; ukiufungua hauna huruma – bunduki*

Sitiari zingine zilitumiwa kueleza sifa au muundo wa vifaa kwa mfano katika kitendawili kifuatacho cha (39) cha Waswahili:

### **Kitendawili (39)**

**Waswahili:** Dada yangu ana tako moja tu – bunduki

Kitendawili hiki kimeegemea kwa mhimili unaoeleza kwamba urejelezi huo huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo kukipa kitendawili hicho nguzo za kitamaduni. Urejelezi huo unajengwa kutokana na viashirii vya utamaduni na tajriba ya maisha kwa hivyo matumizi ya neno ‘tako’ na ‘dada’ ni maneno yaliyozoeleka katika jamii hiyo ndipo yakatumiwa kama kiashirii cha bunduki. Bunduki huwa na umbo la paba moja linalofanana na tako.

Vyombo vingine vilivyoambatana na majilio ya Wazungu ni nyambizi au sabmarini ya vita. Hiki ni chombo kinachosafiri chini ya maji na ambacho hutumiwa aghalabu kutangulia meli za vita. Chombo hicho kililetwa Mwambao wa Pwani na Wazungu waliokuwa na lengo la kuwaondoa Wareno waliokuwa wametawala sehemu hii. Kwa wakati huo, mwaka wa 1600, Wareno walikuwa wamebaki wachache na biashara yao ilikuwa imeanza kuporomoka ndiposa Wazungu wakaona bora waitawale sehemu hiyo (Ochieng, 1985). Majilio ya chombo hicho yalisababisha kuwepo kwa sitiari zilizolingana nacho, ndiposa Waswahili wakabuni kitendawili chenye sitiari ya ‘samaki’ inayowakilisha nyambizi:-

### **Kitendawili (40)**

**Waswahili:** Samaki wangu akiwa majini huenda chini kwa chini tu – nyambizi

Hali iyo hiyo ilidhihirika pia katika sitiari zilizo katika vitendawili vya Abanyala. Kwa mfano katika kitendawili (41):

#### **Kitendawili (41)**

**Abanyala:** *Omusungu ketiye musiuno – esikombe*

**Tafsiri yake:** Mzungu amejishika kiunoni – kikombe

*Kamusi Sanifu ya Kiswahili ya TUKI* (2013), inaeleza kikombe kuwa chombo cha kauri, chuma, madini kitumiwacho kwa kunywea. Jamii ya Abanyala inaamini kuwa majilio ya wazungu yaliambatana na vyombo mbalimbali, kikombe kikiwa kimoja kati yavyo. Hali hiyo iliwapanya Abanyala kuunda kitendawili chenye sitiari ya ‘mzungu’ aliyejishika kiunoni ili kukirejelea.

Majilio ya Waarabu yalileta mabadiliko ya sitiari zilizotumiwa katika vitendawili vya Waswahili. Farsi (1958), anaeleza kuwa kabla ya kuja kwa wageni kutoka nje ya bara hili, ‘bibu mweupe’ ni sitiari iliyotumiwa kurejelea machicha ya nazi. Hii inaonyesha kuwa jamii hii ilikuwa haijaingiliwa na athari za nje. Baada ya kuja kwa Waarabu, sitiari hiyo ilibadilika na kuwa ‘Mwarabu’ kama ilivyo katika kitendawili (42):

#### **Kitendawili (42)**

**Waswahili:** *Mwaarabu wangu nimemtupa biwini - machicha ya nazi*

Baadaye sitiari hiyo ilibadilika tena na kuwa ‘Mzungu’ hii ilikuwa baada ya Wazungu wakoloni kutamalaki sehemu za Mwambao wa Pwani (Khatibu, 1978). Kitendawili kilichotaja neno hilo ni kama hiki kifuatacho (43):

### **Kitendawili (43)**

**Waswahili:** Mzungu wangu katupwa jalalani - machicha ya nazi

Kwa hivyo 'Mwaarabu' na 'Mzungu' katika vitendawili hivyo vya (43) na (44), yametumiwa kurejelea athari za tawala za kigeni zilizoshuhudiwa mwambao wa Pwani.

Hatua iyo hiyo ilishuhudiwa katika jamii ya Abanyala ambao baada ya majilio ya Wazungu na kutamalaki sehemu za magharibi mwa nchi, walibuni vitendawili vyenye sitiari zilizomrejelea na kumdhalilisha mtu mweupe, vitendawili (44) vinatoa mifano hiyo:-

### **Vitendawili (44)**

**Abanyala:** *Omusungu arengerera mwidirisha – amamira*

**Tafsiri yake:** Mzungu anachungulia dirishani – kamasi

**Waswahili:** Wazungu wawili wanachungulia dirishani – kamasi

Ukichunguza tundu za pua hasa za mtu mwenye mafua si ajabu kuona makamasi yakichungulia. Sitiari ya mzungu katika vitendawili vya jamii hizi, ilitumiwa kuonyesha kuwepo kwa mifumo ya kihistoria ya wazungu ndiposa mhimili ukaeleza kuwa ishara huwakilisha viashiriwa fulani na uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni. Ishara hizo zinafungamana na mazingira ambamo vitendawili hivyo vimechimbuka.

Nadharia mbalimbali zimebuniwa na wanajamii kuhusu asili ya funza nchini Kenya. Kulingana na uchunguzi uliofanywa na *Ahadi Kenya Trust* (2012), funza waliletwa nchini Kenya na wakoloni kama njia ya kibiolojia ili kudumaza juhudi za waliokuwa wakipigania

uhuru kwa wakati huo. Utafiti huo unaeleza kwamba wapigania uhuru walilishwa vitu ambavyo vilisababisha kudumaa kwa akili. Hali iyo hiyo, ndiyo ambayo humkumba yeyote aliye na funza kwa sababu, funza hunyonya damu na kusababisha upungufu wa damu mwilini. Baadaye, hewa ya oksijeni hupungua akili na kusababisha kudumaa kwa akili ya anayehusika. Tukio hilo, lilisababisha jamii ya Waswahili na Abanyala kubuni vitendawili vyenye sitiari za hali hiyo. Kwa mfano katika kitendawili (45) kifuatacho:-

### **Kitendawili (45)**

**Abanyala:** *Omusungu kandikitia – enyende*

**Tafsiri yake:** Mzungu ananitekenya – funza

Funza ni mdudu mdogo kama kiroboto ambaye huingia katika miguu ya watu au wanyama. Katika kitendawili hiki, funza ametumiwa kama kiashirii cha mzungu ambaye anaaminiwa kwamba ndiye aliyekuwa chanzo cha wadudu hao. Wadudu hao wanapomvamia mtu popote mwilini, huanza kwa mwasho sawa na kutekenya na baadaye kuhisi maumivu. Ndiposa nadharia inayoongoza utafiti huu ikaeleza kwamba ishara huwakilisha viashiriwa fulani. Uhusiano kati ya ishara na vishiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni (Pierce, 1977). Tukio hilo lilitokea baada ya wakoloni kutamalaki nchini, mifano hii ilionyesha kuwepo kwa mifumo ya kihistoria iliyoandamana na majilio ya Waarabu na Wazungu.

### **3.3 Sitiari kama kiashirii cha sayansi ya kimazingira**

Kutokana na utafiti huu, sitiari zilizobainika katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili, zilitumiwa kurejelea mambo yaliyo katika mazingira. Sitiari hizo hutumiwa katika vitendawili kutokana na tajriba za watu na jinsi wanavyokabiliana na mazingira

yanayowazunguka (Momanyi 2006). Ndiposa mhimili wa nadharia ya semiotiki ukaeleza kuwa urejelezi huo hujengwa kutokana na viashirii vya utamaduni unaorejelewa na tajriba ya maisha. Urejelezi huo huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo kuipa kazi fulani nguzo za kitamaduni. Baadhi ya vitendawili vyenye sitiari zilizotumiwa kurejelea mambo ya kimazingira ni kama vile katika vitendawili (46) vifuatavyo:-

#### **Vitendawili (46)**

**Abanyala:** *Baba arira nikenyala – mvua*

**Tafsiri yake:** Babu analia akikojoa – mvua

**Waswahili:** Babu hupiga kelele akojoapo – mvua

Mvua ni matone ya maji yanayodondoka kutoka kwenye mawingu, mara nyingi mvua huambatana na kelele nyingi. Mzee Francis Watitwa wa jamii ya Abanyala alieleza kwamba kwa vile babu au baba ana uwezo mkubwa katika familia ndiyo maana mvua ambayo inaaminiwa kuwa na uwezo mkuu (kimatumizi) pia, ikatumiwa kumwakilisha baba. Kwa hivyo sitiari ya baba ama babu kuhusishwa na mvua zilionyesha jinsi wenye jamii hizi walivyojikusisha na mazingira yao.

Kutokana na utafiti huu, ilibainika kuwa baadhi ya sitiari zilitumiwa kurejelea kuzaliwa kwa viumbe. Sitiari hizo zimeuficha ujauzito kwa kuuhusisha na kuwinda ama kukwea mti, kwa mfano katika vitendawili (47):

#### **Vitendawili (47)**

**Abanyala:** *Nachia okhuyima, engochwa nditira solo si – okhuba asicho*

**Tafsiri yake:** Nilienda kuwinda lakini sijui nitamwinda mnyama yupi – ujauzito

**Waswahili:** Nimepanda mti lakini sijui utazaa matunda gani – ujauzito

Kwa kawaida, haiwezekani kutabiri mapema mwanamke atajifungua mtoto wa aina gani anaposhika mimba. Vilevile haibainiki ikiwa mtu ameukwea mti ataushuka vipi? Na yeyote anapoenda kuwinda haibainiki atampata mnyama yupi? ‘Mnyama’ katika kitendawili cha Abanyala na ‘matunda’ katika kitendawili cha Waswahili yametumiwa kuashiria mtoto ambaye ni fumbo kwa mamake au jamii kwa sababu haijulikani atazaliwa lini na atakuwa wa jinsia ipi? Kwa hivyo sitiari zinaweza kutumiwa kuashiria sayansi ya kimazingira.

### **3.4 Sitiari kama kiashirii cha mchapuko wa teknolojia**

Mapinduzi ya viwanda katika nchi za bara Ulaya yaliyotokea kati ya miaka ya 1750 na 1850, yalisababisha mchapuko wa teknolojia mbalimbali kupenyeza katika nchi nyingi barani Afrika hususan mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20. Mataifa ya Ulaya kama vile Ujerumani, Uingereza, Ubelgiji, Ufaransa na mengineyo tayari yalikuwisha kuimarisha viwanda vilivyohitaji malighafi. Kwa hivyo wakaangazia bara la Afrika kama behewa lililosheheni malighafi ya kuwafaa (Kiruthu na wengine, 1996).

Hili lilipelekea mataifa hayo kung’ang’ania bara hili na kuligawa katika mipaka inayotangaza utawala wao. Mfumo wa kiistamari uliposhadidi barani humu, baadhi ya teknolojia ngeni zililetwa ikiwemo mitambo na mashine za kuzalisha mali. Mitambo hiyo basi ikachukua nafasi ya watumwa hasa baada ya marufuku kutolewa dhidi ya ununuzi na uuzaji wa watumwa ulimwenguni. Kutokana na hali hiyo baadhi ya vitendawili kama (48) vyenye sitiari zinazohusiana na hali hiyo viliundwa.

### **Kitendawili (48)**

**Waswahili:** *Watwana wangu hawalalamiki, hata wapewe kazi ngumu vipi –mitambo*

Mitambo ni mashine ya kazi. Kwa kawaida mitambo haichoki wala kulalamika hata kazi ikiwa ngumu kiasi gani. Katika kitendawili hicho, watwana wamehusishwa na mitambo ambapo mara nyingi mitambo hufanya kazi lakini hailalamiki. Teknolojia hii haikusambaa tu Pwani, bali barani pia. Kwa mfano, jamii ya Abanyala iliweza kubuni vitendawili vyenye sitiari hizo za kiteknolojia kama kifuatacho cha (49):-

### **Kitendawili (49)**

**Abanyala:** *Ekorokocho liange lichuye ebichuma – emuri chie sibiriti*

**Tafsiri yake:** Lori langu limejaa chuma – njiti za kiberiti

Katika kitendawili hiki (49), njiti za kiberiti zimetumiwa kuashiria chuma zilizo ndani ya lori. Hali hiyo inaegemea kwenye mhimili unaoshikilia kuwa ishara huwakilisha viashiriwa fulani, uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni. Dhana iliyomo mawazoni mwa wanajamii ni lori kuwa na chuma ambazo zimelinganishwa na njiti za kiberiti. Hayo yote yaliweza kutokea kwa sababu ya mchapuko wa teknolojia.

Isitoshe sitiari ya magurudumu ya gari yaliweza kulinganishwa na watoto. Kitendawili hiki kilitambulika katika jamii ya Abanyala na vilevile Waswahili. Gari linapokwenda, magurudumu yake huzunguka, yale ya nyuma huwa kama yanafukuza yale ya mbele ingawa hubakia palepale.

### **Vitendawili (50)**

**Abanyala:** *Abana bange bane balondananga wuli nyanga ne sibatiranga tawe – amagurudumu*

**Tafsiri yake:** Watoto wangu wanne wanafukuzana kila siku na hawakamatani kamwe – magurudumu

**Waswahili:** Watoto wane ambao daima hufukuzana lakini hawakamatani – magurudumu

Mifano hii inadhihirisha kuwa sitiari katika vitendawili ilitumiwa kuonyesha jinsi jamii hizi zilivyopiga hatua kiteknolojia.

### **3.5 Sitiari kama kiashirii cha chakula**

Chakula ni kitu chochote kinacholiwa ambacho huupatia mwili nguvu (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2013). Utafiti huu ulibaini kwamba sitiari nyingi zilizohusishwa na vyakula vya jamii za Abanyala na Waswahili, zilitaja ugali. Kulingana na *Kenya Information Guide* (2013), ugali unajulikana kama ‘obusuma’, ndicho chakula cha kiasili cha Abaluyia. Ugali unatengezwa kutokana na unga wa mahindi au mhogo. Hata ingawa Abaluyia hula vyakula vingine, chakula hakijakamilika ikiwa ugali haupo kwa hivyo, vitendawili mbalimbali vimebuniwa Abanyala vyenye sitiari zinazoashiria ugali. Kwa mfano (51):-

### **Vitendawili (51)**

**Abanyala:** *Ikhala eyi nase nikhale eyi khukhupe etulo lino – owusuma*

**Tafsiri yake:** Kaa huko nami huku tupige mlima huu – ugali

**Waswahili:** Kaa huko nami nikae huku tupande mlima – ugali

Kwenye vitendawili hivyo, neno mlima ni sitiari ya ugali, Mzee Kalukhana wa jamii ya Abanyala, alieleza kuwa ugali ndicho chakula kinachopendwa sana na Abanyala. Iliaminiwa kuwa ugali unampa mtu nguvu ndiyo maana unaliwa mchana na hata jioni. Hali hiyo iliwafanya Abanyala kubuni vitendawili vyenye sitiari inayohusiana na ugali. Mbali na hayo, wanajamii walifaa kuwa pamoja wanapokula ugali, kwa hivyo lilikuwa kama jambo la jambo la ushirika.

Sitiari zingine zilizotumiwa katika vitendawili vya Abanyala zilionyesha kuwa mboga aina ya 'Mlenda' ilitumiwa kama kitoweo kwa kulia ugali wa mhogo (Mumali Ndombi). Kwa hivyo, kitendawili kama kifuatacho (52) kinaonyesha jinsi ugali na 'Mlenda' unavyoshikama wakati wa mlo.

### **Kitendawili (52)**

**Abanyala:** *Yema engerekha neme engerekha khukamulane – owusuma wo mwoko nomuchere*

**Tafsiri yake:** Simama ng'ambo nisimame ng'ambo tushikane – ugali wa mhogo na mlenda

Sitiari zingine zilionyesha kwamba viazi vitamu vilikuwa miongoni mwa vyakula vilivyoliwa na jamii hizi mbili. Kwa mfano katika jamii ya Waswahili, sitiari ya ng'ombe katika kitendawili hiki (53), '*Ng'ombe wa babu walala mkia nje – viazi vitamu*', inahusishwa na viazi vilivyo (ardhini) udongoni. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya semiotiki, ishara huwakilisha viashiriwa fulani, uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni, ndio maana kwa vile viazi huwa chini ardhini na kitu kinachoonekana juu ya ardhi ni mashina ya mmea huo ambayo huwa marefu na membamba kama mkia, yamelinganishwa na mkia wa ng'ombe.

Mfano mwingine unaoonyesha viazi kuwa sehemu ya chakula cha jamii ya Waswahili ni huu (53) ufuatao: ‘nilipitisha mkono wangu chini ya ardhi nikamshika beberu mkubwa sana – kiasi kikuu’. Mtu anapochimba viazi vikuu ardhini hutumia kifaa cha kuchimbia pamoja na mikono yake ambayo huitoa viazi vyenyewe. Katika kitendawili hiki cha (53), ‘beberu mkubwa’ ametumiwa kama sitiari ya kiasi kikuu. Ishara hizo mbalimbali zilizotumiwa, zinafungamana na mazingira ambamo vitendawili hivyo vinachimbuka vile unavyoeleza mhimili wa nadharia inayoongoza utafiti huu kuwa urejelezi huo huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo kukipa kitendawili hicho nguzo za kitamaduni.

Katika jamii ya Abanyala, kitendawili kilichoonyesha sitiari yenye uhusiano na viazi ni hiki (54):

#### **Kitendawili (54)**

**Abanyala:** *Kukhu afulama musipwono – efukho musipwoni.*

**Tafsiri yake:** Nyanya ameinama shambani – fuko kwenye shamba la viazi vikuu

Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2013), fuko ni mnyama kama panya mwenye macho madogo aishiye shimoni. Mzee Watitwa, alieleza kuwa mnyama huyo hupenda kuishi kwenye shamba la viazi, na hula viazi, kwa hivyo mnyama huyo alihusishwa na nyanya kwa ajili nyanya (wanawake) ndio wanaochimba viazi huku wakiwa wameinama. Cha mno ni kuwa viazi vilikuwa sehemu ya chakula cha Abanyala.

Kwa ajili ya mifano iliyodondolewa, baadhi ya sitiari zinazotumiwa katika vitendawili, zinatumiwa kuonyesha vyakula vinavyotumiwa na jamii za Abanyala na Waswahili.

### 3.6 HITIMISHO

Katika sura hii, maudhui katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili yameelezwa. Utafiti huu ulitambua kuwa sitiari mbalimbali zina maudhui tofauti tofauti, maudhui ambayo yaliangaziwa katika sura hii ni kama vile: sitiari kama kiashirii cha kifo ama ugonjwa. Mifano mbalimbali ilijitokeza katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili kama vile, mgonjwa wa ndui alifananishwa na fenesi, ugonjwa wa UKIMWI ulifananishwa na jitu zaidi ya hayo, sitiari zilionyesha kwamba baada ya kifo, hakuna kurudi hali hiyo ililinganishwa na jani linapoanguka kutoka mtini.

Fauka ya hayo, sitiari katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili ziliashiria kuwepo kwa mifumo ya kihistoria iliyoshuhudia majilio ya wageni. Wageni waliorejelewa hasa walikuwa Wazungu na Waarabu, majilio yao yalishuhudia kuletwa kwa vyombo mbalimbali ambapo sitiari mbalimbali zilizolinganishwa na vyombo hivyo ziliundwa. Sitiari zizo hizo ndizo zilizotumiwa katika vitendawili vya jamii zao vile unavyoeleza mhimili wa nadharia inayoongoza utafiti huu kuwa urejelezi huo huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo kuvipa vitendawili hivyo nguzo za kitamaduni. Ndiyo maana kiashirii huweza kuwa kile kile bali kinachorejelewa kikawa tofauti kwa mujibu wa utamaduni na tajriba ya maisha.

Sitiari zingine zilitumiwa kama kiashirii cha sayansi ya kimazingira. Sitiari nyingi zilitumiwa kuonyesha jinsi ambavyo jamii hukabiliana na mazingira kwa mfano 'babu' ni neno lililotumiwa kuashiria mvua na dhana ya kuwinda na kukwea mti, ililinganishwa na ujauzito.

Hali kadhalika swala la mchapuko wa kiteknolojia katika jamii lilielezwa kupitia kwa sitiari ambapo mitambo na mashine tofauti tofauti ziliundwa ili kuchukua nafasi ya watumwa, hali

hiyo ilisababisha vitendawili vyenye sitiari zinazohusiana na hali hiyo kuundwa. Kwa mfano watwana walilinganishwa na mitambo, chuma ndani ya lori zikalinganishwa na njiti za kiberiti na magurudumu yakalinganishwa na watoto wanne wanaofukuzana.

Isitoshe sitiari zingine ziliashiria chakula cha kiasili cha jamii za Abanyala na Waswahili. Viasi vikuu na ugali ni vyakula ambavyo vilijitokeza mno katika sitiari zilizotumiwa katika vitendawili vyao haya yalibainika kwa mujibu wa mhimili unaoeleza kuwa ishara huwakilisha viashirii fulani na uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni. Kwa hivyo sitiari katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili zina maudhui mapana.

## SURA YA NNE

### DHIMA YA VITENDAWILI KATIKA JAMII ZA ABANYALA NA WASWAHILI

#### 4.0 UTANGULIZI

Sanaa ya vitendawili huibuliwa kutoka katika bongo za watu na kutolewa katika miktadha maalum, aidha sanaa hii hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine (Momanyi, 2006). Dhima muhimu ya vitendawili ni kufunza na kuyaweka bayana mambo yanayothaminiwa na jamii. Kwa sababu hiyo, watu tofauti tofauti hutumia vitendawili katika mawasiliano yao kwa ajili ya malengo mbalimbali. Kwa hivyo, sura hii imeshughulikia sababu zinazofanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao. Utafiti huu ulitambua kuwa, sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumiwa vitendawili katika mawasiliano yao ni kama vile: kuchochea udadisi, kukuza maadili, kuelimisha, kudhihaki, kigezo cha kusawiri maisha ya jamii, chombo cha kuburudisha na njia ya kuwasilisha ujumbe kwa muhtasari.

#### 4.1 Kitendawili kama chombo cha kuchochea udadisi

Watu wengi hutumia vitendawili kwa maksudi ili viwe kichocheo cha kutafakarisha. Kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki, ishara huwakilisha viashiriwa fulani, uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni (Eschbach, 1983). Kwa hivyo hadhira inapokumbana na vitendawili, hupiga bongo ili iweze kupata fasiri dhahiri kwanza ndipo baadaye iweze kujiuliza sababu ya msingi ya kutumiwa kwayo katika muktadha husika, hadhira hushiriki katika upokezi wa ujumbe katika kutafakari zaidi. Wanafunzi wa shule za misingi za jamii za Abanyala na Waswahili, wengi wao walikiri kuwa vitendawili huwachemsha bongo na kuwatafakarisha wakati vinapotegwa, kwamba vitendawili ni njia

nzuri ya kuujaribu uwezo wao wa kuyakumbuka mambo fulani, matukio maalum na mambo yanayohusiana na historia na mazingira yake. Hali hiyo inatokana na uzoefu wa kutafuta kiini cha kitendawili ambao hujenga tabia ya kutaka kufichua jambo lililofichika. Kwa kujaribu kupata jibu la fumbo katika kitendawili, wanajamii huimarisha ari yao ya kutafiti mambo ili kubaini kiini chake. Kwa mfano:

### **Kitendawili (55)**

**Abanyala:** *Sindariakho omunju yesiyesi ta – efwa / enjala*

**Tafsiri yake:** *Simuogopi mtu yeyote – kifo/ njaa*

**Waswahili:** *Hamwogopi mfalme wala bawabu – kifo / njaa*

Kitendawili hiki (55) kinamchochea anayetegewa kutafuta kitu au hali katika mazingira yake au katika maisha yake ambacho daima hakitishiki na chochote na hutokea tu bila kizuizi chochote. Utambuzi wa anayetegewa lazima utamwelekeza kwamba, daima binadamu wote lazima watakufa. Hakuna anayeweza kukiepuka kifo awe mfalme au mtu wa kawaida au wa tabaka la chini bila ya ubaguzi wala hofu kifo huchukua tu watu. Papo hapo atagundua jibu la kitendawili hicho kuwa ni kifo kwa kutegemea muktadha. Ndiposa nadharia ya semiotiki ikaeleza kuwa, urejelezi huu huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji. Kwa njia hiyo, huipa kazi fulani nguzo za kitamaduni. Ndiyo maana kiashirii huweza kuwa kilekile bali kinachorejelewa kikawa tofauti kwa mujibu wa utamaduni na tajriba ya maisha.

Vitendawili vina nafasi ya kuchochea ari kuhusu sayansi ya kimazingira. Hii ni kwa sababu vitendawili vingi huchimbuka kutokana na mazingira na ndio maana viashirii vinavyotumiwa

katika vitendawili hivyo, hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine lakini kinachorejelewa, huwa ni kilekile (Miruka, 1994). Vitendawili vifuatavyo (56) kutoka katika jamii za Waswahili na Abanyala, vitaichochea hadhira kufaragua maswala ya kijamii na vilevile maswala ya kimazingira, baada ya kuyaoanisha, ndipo atakapokitegua kitendawili hiki cha (56).

### **Vitendawili (56)**

**Waswahili:** *Baba, mayi na baana muchiaye? – Enyanga, omwesi nende eng'inang'ini*

**Tafsiri yake:** Baba, mama na watoto mnaenda wapi? – Jua, mwezi na nyota

**Waswahili:** Babu, nyanya na wajukuu wake – jua, mwezi na nyota

Uzoefu wa kutafuta kiini cha kitendawili kama hiki (56), hujenga tabia ya kutaka kufichua jambo lililofichika kwa kujaribu kupata jibu la fumbo katika kitendawili. Kwa njia hiyo wanajamii huimarisha ari yao ya kutaka kutafiti mambo ili kubaini kiini chake. Ndio maana nadharia inayoongoza utafiti huu ikaeleza kwamba sifa bainifu za kisemantiki hutuwezesha kupata picha fulani katika kazi za kifasihi kwa kuibua fahiwa za maana (Barthes, 1977).

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2013), inaeleza kuwa jua ni gimba kubwa lenye nuru kali lililoko angani ambalo hutoa mwanga na joto. Katika kitendawili (56), jua limelinganishwa na 'baba' kwa ajili ya uwezo alionao katika jamii. Mwezi ni gimba mojawapo linalozunguka dunia mara moja kila siku 28 na linang'ara usiku. Mwezi umelinganishwa na mama. Nyota ni gimba lenye nuru lililoko angani ambalo halizunguki bali huzungukwa na baadhi ya sayari na nuru yake huonekana zaidi wakati wa usiku. Nyota zimelinganishwa na watoto katika jamii ambao mara nyingi hawana mamlaka zaidi ikilinganishwa na wazazi wao (Mzee Wawire).

Kwa mkondo huo, itampasa anayetegewa awe na uwezo wa kudadisi zaidi ili aelewe kinachorejelewa.

Kutokana na mifano iliyotolewa ni dhahiri kwamba vitendawili hutumiwa na Waswahili na Abanyala ili kukuza uwezo wa kudadisi na kuchemsha bongo.

#### **4.2 Kitendawili kama chombo cha kukuza maadili**

Vitendawili huweza kufunza mienendo na kanuni zinazokubalika katika jamii mbali na kusawiri maisha ya jamii. Mzee Francis Watitwa na Mama Agnes Liaka, walieleza kwamba vitendawili vilitumiwa sana katika mawasiliano ili kufunza wanajamii maadili. Kwamba vitendawili huwa na utaratibu fulani unaofuatwa na wale ambao wanashiriki wanapaswa kuuheshimu na kuuzingatia. Hii ilikuwa njia moja ya kuadilisha kuwa kila jambo maishani lina kaida zake ambazo ni lazima ziheshimiwe. Walifafanua kwamba, kabla ya kutega kitendawili chochote, lazima mtegesi ajitambulisha kwa hadhira kwa kuwaeleza jina lake, baba yake, babu yake, ukoo wake miongoni mwa maswala mengine ya kibinafsi. Isitoshe, kitendawili kinachotegwa, huwa na maadili fulani yanayopaswa kutiliwa maanani kwa mfano kitendawili (57):-

#### **Kitendawili (57)**

**Abanyala:** *Nali nesunga, nesunga yange natong'a nayo – engamia*

**Tafsiri yake:** Nilikuwa na maringo, na maringo hayo nilibaki nayo – ngamia

Kitendawili hiki (57) kinasisitiza kuwa haimfai mtu kuwa na maringo au majivuno mengi, huenda hayo majivuno yakamsababishia maafa katika maumbile yake vile maringo ya ngamia yalivyomsababishia kuwa na nundu mgongoni.

Kwa upande mwingine, swala la maadili lilitiliwa mkazo katika jamii ya Waswahili, waliendeleza jambo hilo la maadili kupitia kwa kitendawili kama kifuatacho cha (59):

#### **Kitendawili (58)**

**Waswahili:** Nyumbani mwetu kuna papai lililoiva lakini nashindwa kulila – kaka hawezi kumwoa dada yake

Katika jamii nyingi zikiwemo jamii za Waswahili na Abanyala, ndoa kati mtu na dadake zimeharamishwa, ni mwiko. Kitendawili kama hiki (58) kikitegwa, hadhira inafahamu kwamba haipaswi kuwa na uhusiano wowote wa kimapenzi na jamaa zao.

Fauka ya hayo, vitendawili vilitumiwa na jamii za Abanyala na Waswahili ili kuwatahadharisha dhidi ya mambo yanayoweza kuangamiza jamii. Vitendawili vingi vilikashifu tabia ya kujihusisha na nyendo mbaya. Kwa mfano, katika jamii ya Abanyala kitendawili kifuatacho (59) kinatahadharisha watu dhidi ya kuona watu wanakimbia na bila ya kujua sababu inayowafanya wakimbie, yeyote naye anaanza tu kutoroka. Hali kama hiyo huenda ikamsababishia anayetoroka bila kufahamu anachotorokea madhara makubwa (Mzee Francis Watitwa).

#### **Kitendaawili (59)**

**Abanyala:** *Baba akhina ne abana bemire – amasanja ke chemwa no mukoko*

**Tafsiri yake:** Baba anacheza na watoto wamesimama – matawi ya ndizi na mgomba wake

Upepo unapovuma matawi ya ndizi huchezacheza ilhali mgomba wake husimama. Funzo lililopo ni kwamba wezi wanapofukuzwa, wao ndio hutoroka zaidi ili wasishikwe. Kwa

hivyo jamii inatahadharishwa dhidi ya kujiingiza katika vitendo viovu kwani huenda vikawadhuru.

Mifano hii iliyodondolewa inaonyesha bayana kuwa vitendawili hutumiwa na jamii hizi ili kukuza maadili.

#### **4.3 Kitendawili kama chombo cha kuelimisha.**

Vitendawili huwa na upana mkubwa wa kimaudhui jambo ambalo huvifanya viwe nyenzo kubwa ya kuelimisha jamii. Maswala mengi yanayohusu mazingira hujumuishwa katika vitendawili. Hali hiyo imevifanya vitendawili kuwa na uwezo mkubwa wa kuelimisha watu kuhusu mazingira yao (Matei, 2011). Kwa mfano katika kitendawili (60), kuenea na kujaa kwa nyota mbinguni usiku na inapofika asubuhi zinatoweka kwa sababu ya mwanga wa jua, kumelinganishwa na namna mpunga ambao huzaa mashuke na baada ya kukobolewa hutoa mchele.

#### **Kitendawili (60)**

**Waswahili:** Alianika mpunga wake alipoamka haupo – nyota

Fauka ya hayo, katika mtazamo wa jamii nyingi za Kiafrika, jua hulinganishwa na mwanamme, mwezi na mama nazo nyota huonekana kama watoto. Hii ni kwa misingi ya nafasi wanazopewa katika jamii kwa ajili hiyo, Waswahili walibuni kitendawili kifuatacho (61) kuelezea hali hiyo. Kitendawili hiki kinaeleza kwamba, jua linapotoka, mwezi na nyota hazionekani, huonekana tu usiku wakati jua halipo.

#### **Kitendawili (61)**

**Waswahili:** Akitoka mkewe na watoto hulala – jua

Kutokana na vitendawili hivyo, maswala ya kisayansi yanayohusu jua, mwezi na nyota wanajamii huyafahamu kupitia kwa vitendawili kama hivyo.

Mbali na kujifunza mambo tofauti tofauti yanayotajwa katika vitendawili, mtu akikosa jibu la kitendawili, haadhibiwi zaidi ya kutoa mji akishataja tu, hupewa jibu. Kwa hivyo, katika vitendawili, kukosa jibu na kupata jibu ni njia ya kuelimisha (Matei, 2011).

Vitendawili vingi hutaja nambari za vitu mbalimbali kwa njia hiyo, watoto hujifunza kwa urahisi namna ya kuhesabu (Miruka, 1994). Kuna vitendawili vinavyohusu sehemu za mwili wa binadamu, katika maelezo ya vitendawili hivyo, idadi kamili ya sehemu hizo hutajwa kama vile: idadi ya masikio, miguu, macho, vidole na pua miongoni mwa sehemu zingine. Kwa mfano, kitendawili (62) kifuatacho cha Abanyala, kimetumia sitiari ya watoto watano kurejelea vidole vitano vya mikono:

#### **Kitendawili (62)**

**Abanyala:** *Endi nabana bange bachanu bakholasa emirimo – enjala chie mikhono.*

**Tafsiri yake:** Nina watoto wangu watano wanafanya tu kazi – vidole vya mikono

Waswahili walibuni kitendawili kifuatacho kinachotaja macho kwa kutumia sitiari ya ndugu wawili wanaofanana lakini hawatembeleani kwa lengo la kurahisisha kuhesabu miongoni mwa watoto. Macho huwa yanafanana isipokuwa kwa ajali au hitilafu za kimaumbile lakini hayatembeleani. Licha ya kukitegua kitendawili hiki, hadhira pia hujifunza namna ya kuhesabu. Kitendawili chenyewe ni hiki kifuatacho (63):

#### **Kitendawili (63)**

**Waswahili:** Ndugu wawili wanafanana lakini hawatembeleani – macho

Nao Abanyala walitumia kitendawili kifuatacho (64) kuhusu macho, kitendawili hiki kinaeleza jinsi ambavyo watu watatu wanaanza safari kwa pamoja na wawili wanatangulia kufika. Wawili hao wanaotangulia kufika ni macho mawili na wa tatu ni mtu mwenyewe binafsi anayaenda safari hiyo.

#### **Kitendawili (64)**

**Abanyala:** *Khuli batachu, nikhuchakira khulala olukendo njanu ochangirira okhwola – emoni*

**Tafsiri yake:** Tuko watatu, tukianza pamoja kwenda safari nani anatangulia kufika – macho Ushirikiano katika jamii ni jambo ambalo lilitiliwa maanani. Maendeleo mengi katika jamii yamefikwa kwa sababu ya ushirika. Kwa sababu hiyo, vitendawili mbalimbali hutumiwa na watu ili kuhimiza watu washirikiane. Kwa mfano, vitendawili (65) vifuatavyo vya Abanyala na Waswahili vilitoa funzo kwamba ni lazima watu washirikiane kwa kila jambo ili waweze kufaulu, chambilecho “jifya moja haliinjiki chungu.”

#### **Kitendawili (65)**

**Abanyala:** *Endi nabana bange batachu mulala nachulakho sibakhola ekasi ta – amaika*

**Tafsiri yake:** Nina watoto wangu watatu, mmoja akitoka hawafanyi kazi kamwe – mafiga

**Waswahili:** Nina watoto watatu, akiondoka mmoja kazi haifanyiki – mafiga

Jifya moja linapoondolewa na yabaki mawili, chungu au sufuria haitaweza kuinjikika vyema mekoni, kwa hivyo ushirika wa wote unastahili kuwepo miongoni mwa wanajamii.

Kupitia kwa mifano iliyotolewa, vitendawili hutumiwa na jamii za Waswahili na Abanyala ili kuelimisha jamii maswala mbalimbali. Kwa mfano, maswala ya kimazingira, kuhesabu, ushirikiano, viungo vya mwili miongoni mwa maswala mengine.

#### 4.4 Kitendawili kama njia ya kudhihaki.

Uteuzi wa sitiari za vitendawili zina sifa ya kudhihaki watu fulani kwa kuyatumia majina yao kama msingi wa ulinganishi kwenye muundo wa kitendawili kinachohusika. Hali au tabia hasi katika jamii ndizo zinazokashifiwa. Kwa mfano katika jamii hizi za Abanyala na Waswahili, mzungu amekashifawa (Ochieng 1985). Kutokana na hali hiyo, Waswahili waliweza kubuni vitendawili vinavyoeleza hali hiyo. Kwa mfano, katika kitendawili cha Waswahili kilichotolewa awali '*mzungu katupwa jalalani – machicha ya nazi*'. Kitendawili hiki, kimelinganishwa machicha ya nazi na mzungu (kutokana na weupe wake), kwa kiasi fulani, kuna dhihaka kwenye usemi huo inayoonyesha hisia fulani kuwahusu wazungu.

Hali kadhalika, kitendawili kiki hiki kilibadilika kwa kuegemea upande wa kuwadhihaki wageni waliozuru mwambao wa Pwani hasa Waarabu na Wazungu. Kabla ya kuja kwa wageni hao kama vile Wareno, Wazungu, Wafaransa, Waarabu, Waajemi na Wagriki miongoni mwa wengine (Ochieng, 1985). Sitiari zilizotumiwa katika kitendawili hicho kabla ya kuja kwa wageni hao zilikuwa kama ilivyo katika kitendawili hiki '*bibi mweupe ametupwa miibani*.' Katika mfano huo, jamii hiyo ilikuwa haijaingiliwa na athari za nje. Baada ya kuja kwa Waarabu sitiari za kitendawili hiki zilibadilika na kuwa kama ilivyo katika mfano wa kitendawili cha Waswahili kilichotolewa awali '*Mwarabu wangu nimentupa biwini*.' Baadaye kilibadilika kuwa namna ilivyo katika mfano wa kitendawili '*mzungu katupwa jalalani*.' Hii ni baada ya wazungu wakoloni kutamalaki janibu hizo. Kwa ajili hiyo, kule

kulinganishwa kwa ‘Mzungu na Mwarabu kutupwa jaani,’ ilikuwa ni njia moja ya kuwadhihaki hao wageni ndiposa nadharia ya semotiki ikaeleza kwamba ishara huwakilisha dhana fulani. Uhusiano kati ya ishara na viashiriwa, hujengwa na dhana zilizomo mawazoni.

#### **4.5 Kitendawili kama kigezo cha kusawiri maisha ya jamii**

Utamaduni na hali ya maisha ya watu hujumuisha lugha, dini, mila na desturi, mavazi, chakula na kadhalika. Kila jamii ina njia zake za kuendeleza hali yao ya maisha. Yeyote anayetenda kinyume na matakwa ya jamii hukashifiwa. Matakwa ya kijamii hubadilika kulingana na umri, jinsia na vyeo (Mbarwa, 1989). Kwa sababu hiyo, utafiti huu ulitambua kuwa jamii ya Abanyala hujihusisha na shughuli ya kuwapasha wavulana tohara ndipo waingie katika hatua ya utu uzima (Mzee Wawire). Shughuli hii ilipelekea kubuniwa kwa kitendawili kifuatacho (66):

#### **Kitendawili (66)**

**Abanyala:** *Epilipili manga – omubano kwa bakhebi*

**Tafsiri yake:** Pilipili manga – kisu cha ngariba

Kiashiriwa cha *pilipili manga* ambayo ni kali katika muktadha wa kitendawili hiki ni ukali wa kisu cha ngariba.

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2013), inaeleza kisu kama kifaa kirefu kilichotengenezwa kwa chuma au bati kilicho bapa na chenye ukali upande mmoja kinachotumiwa kwa kukatia. Naye ngariba ni mtu anayefanya kazi ya kutahiri wavulana jandoni. Kutokana na mfano wa kitendawili hiki (66) ‘pilipili manga- kisu cha ngariba,’ kinapoteywa, hadhira inafahamu kuwa jamii hiyo ya Abanyala hujishughulisha na kuwapeleka vijana wao jandoni.

Shughuli ya kupasha tohara huwa na matukio mbalimbali. Kati ya matukio hayo kuna kupelekwa kwa nyanya mzaa mama. Kulingana na mhimili wa nadharia inayoongoza utafiti huu unaohusu jinsi matukio yanayopatikana katika kazi fulani yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyounda na kuuelewa msuko wa kazi hiyo kwa kuangalia jinsi matukio hayo yanavyofuatana kinathari au kinasibishi, kitendawili kifuatacho (67) kinaeleza hali anayopitia mvulana kabla ya kutahiriwa. Kinaeleza namna ambavyo anayetiwa jandoni hupelekwa kwa nyanya akiwa anacheza njuga kisha akarudi kwao nyumbani kwa shughuli hiyo ya kupashwa tohara. Kitendawili hicho ni:

#### **Kitendawili (67)**

**Abanyala:** *Enjia ewa kukhu ekhuba engita engola ekhuba engita – enyimba*

**Tafsiri yake:** Ninaenda kwa nyanya ninapiga gita ninarudi ninapiga gita – njuga

Vitendawili hivi vinaonyesha bayana kuwa, shughuli ya upashaji tohara hutekelezwa katika jamii ya Abanyala.

Jamii za Waswahili na Abanyala hujishughulisha na ukuzaji wa mimea na ufugaji wa mifugo. Haya yalibainika kupitia kwa vitendawili vyao. Kwa mfano, swala la upanzi wa mahindi liliweza kujitokeza kupitia kwa vitendawili vifuatavyo (68):

#### **Kitendawili (68)**

**Abanyala:** *Abasikari bange bafwaye ekofia chifwanana – owuyefwe wamatumwa*

**Tafsiri yake:** Askari wangu wamevaa kofia zinazofanana – kishungi cha nywele za mahindi

**Waswahili:** Askari wangu wote wamevaa kofia upande – mahindi

Vitendawili hivyo vina sitiari za kofia zinazoonyesha kwamba shughuli za upanzi wa mahindi hutekelezwa katika jamii hizi. Kofia zilizozungumziwa ni kishungi ambacho huonekana kama kimeinama katika upande mmoja wa mahindi.

Ndizi pia zilijitokeza katika vitendawili vya Waswahili na Abanyala, kwa mfano katika jamii ya Abanyala kitendawili kifuatacho (69) kilionyesha kuwa kuna upanzi wa ndizi.

#### **Kitendawili (69)**

**Abanyala:** *Baba akhina ne abana bemire- amasanja kechemwa nomukoko*

**Tafsiri yake:** Baba anacheza na watoto wamesimama – matawi ya ndizi na mgomba wake Mgomba wa ndizi husimama ilhali matawi yake huchezacheza. Kitendawili hiki kina funzo lake maalum funzo linaloelezwa kupitia kwa mmea huo wa ndizi. Nao Waswahili vilevile kupitia kwa kitendawili hiki cha (70):

#### **Kitendawili (70)**

**Waswahili:** Mpini mmoja tu lakini majembe hayaahasabiki – mkungu wa ndizi

Kitendawili hiki kinaonyesha kwamba Waswahili hujishughulisha na upanzi wa ndizi. Kwenye kitendawili hiki, mpini ni sehemu ya kushikia inayowekwa au kupigiliwa kwenye chombo kingine kama jembe, shoka, nyundo au kisu. Na mkungu mmoja huwa na ndizi nyingi sana, ulinganisho huo uliweza kufanikishwa kwa sababu ya kukuza mmea huo. Kupitia kwa mifano hiyo, ni dhahiri kuwa Waswahili na Abanyala hutumia vitendawili katika mawasilino kama kigezo cha kusawiri maisha yao.

#### 4.6 Vitendawili kama chombo cha kuburudisha

Finnegan (1970), Blacking (1971), Nandwa (1976) na Lusweti (1984), wanaeleza kwamba vitendawili ni mchezo wa watoto ambao hulenga kuburudisha. Kauli hiyo inatiliwa maanani na Akivaga na Odaga (1982) wanaoeleza kwamba umuhimu mkubwa wa vitendawili ni kuburudisha ambapo huwapumzisha na kuwapumbaza wanaoshiriki katika utegaji na uteguaji wa vitendawili. Sababu hii ilijitokeza katika jamii za Waswahili na Abanyala. Walikubaliana na maoni kuwa upo umuhimu wa kufurahia fasihi zetu za Kiafrika hususan katika mawanda ya elimu. Lengo lake likiwa kuwafunza wanafunzi wafaulu mtihani na pia waweze kuburudishwa na kulisimuliwa na sanaa hii (P'Bitek, 1973). Kwa hivyo vitendawili katika jamii hizi, vilitumiwa kama njia moja ya kuburudisha sio tu watoto bali pia watu wazima.

Burudani katika vitendawili inatokana na uelewa wa baadhi ya viashirii vinavyotumiwa katika vitendawili na viashirii hivyo huwa vimezoeleka katika utamaduni wa jamii hizo. Ndio maana nadharia inayoongoza utafiti huu ikaeleza kwamba urejelezi huo huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo, kuipa kazi fulani nguzo za kitamaduni. Kwa sababu hiyo, kiashirii huweza kuwa kilekile bali kinachoashiriwa kikawa tofauti kwa mujibu wa utamaduni na tajriba ya maisha.

Utegaji na uteguaji wa vitendawili hufanywa kwa njia inayowafanya wahasika kujipumbaza na kupitisha wakati kwa njia nzuri. Hii ni kwa sababu, umbo la kitendawili limejikita katika mfumo maalum unaohusisha swali na jibu (Finnegan, 1970).

Vilevile, burudani katika vitendawili hutokana na mazingira ambamo vitendawili vyenyewe hutegwa na kuteguliwa. Miruka (1994) anafafanua kwamba, mazingira hayo ni lazima yawe huru na yasiwe na urasmi wowote hivi kwamba kuna kuelewana kati ya wote wanaoshiriki na

hakuna mkubwa wala mdogo. Kwa ajili ya uhuru uliyopo, hakuna swala la kushurutishwa kati ya wote wanaoshiriki kwa sababu wamejitolea kushiriki wao wenyewe binafsi na kikamilifu. Kwa sababu hii, Abanyala na Waswahili hutumia vitendawili katika mawasiliano yao.

#### **4.7 Vitendawili kama mbinu ya kuwasilisha muhtasari wa ujumbe**

Mchango wa vitendawili katika jamii ni kumsaidia mtegaji kusawiri na kuwasilisha ujumbe wake kwa muhtasari. Kwa mfano ujumbe unaohusu umoja katika jamii ni mpana mno. Mtegaji anaweza kutoa maelezo na kuwasilisha ujumbe kupitia kwa mifano inayofahamika na kuifafanua katika kitendawili chake. Kuna uwezekano kwamba mtegaji angetaka kufafanua zaidi mawazo yake lakini kutokana na muda hawezi kufanya hivyo (Mzee Rajab Idi). Kwa sababu hiyo, mtegaji anaweza kutumia kitendawili hiki (71) ‘Nina watoto watatu, mmoja akitoka wengine hawafanyi kazi – meko,’ kwa lengo la kuufumba na kuuwasilisha ujumbe kwa muhtasari. Kwa hivyo matumizi ya sitiari ya ‘*watoto watatu*’ katika kitendawili hiki, imetumiwa kama fupa ambalo huhitaji mnofu. Katika muktadha huo, msomaji hutarajiwa kujitolea maelezo mapana wakati anapokumbana na kitendawili kama hiki. Kwa sababu hiyo, mtegaji huwa ameamua kwa maksudi kutumia kitendawili ambacho kimemsaidia kuwasilisha ujumbe wake kwa muhtasari.

#### **4.8 HITIMISHO**

Sura hii imeshughulikia sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao. Sababu hizo zimeelezwa kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya semiotiki. Mhimili huo unajengwa kutokana na viashirii vya utamaduni unaorejelewa na tajriba ya maisha. Urejelezi huo huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani

vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo kuipa kazi fulani nguzo za kitamaduni. Ndio maana kiashirii huweza kuwa kilekile bali kinachorejelewa kikawa tofauti.

Utafiti huu ulitambua kwamba sababu zinazofuata huwafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao: wanajamii hizi walieleza kuwa vitendawili huchochea ari ya kudadisi. Hii ni kwa sababu, kabla ya kutoa jibu la kitendawili, hadhira ni lazima itafakari kuhusu maswala mbalimbali katika jamii ambayo yanaashiriwa katika kitendawili kilichotegwa.

Mienendo na kanuni zinazokubalika katika jamii hukuzwa kupitia kwa vitendawili. Maswala ya maringo, ndoa zisizokubalika katika jamii ni maswala yaliyojitokeza katika vitendawili vya jamii za Abanyala na Waswahili. Maswala hayo yalikanwa kupitia kwa umbo la ngamia na tunda la papai ambalo haliwezi kuliwa ilhali limeiva na lipo nyumbani.

Utafiti huu pia ulitambua kuwa Waswahili na Abanyala hutumia vitendawili ili kuelimisha jamii. Haya yalibainika kupitia kwa utaratibu unaofuatwa wakati wa kutega na kutegua vitendawili. Ushirikiano, namna ya kuhesabu kulifanikishwa katika jamii hizi kupitia kwa vitendawili vyao vilivyotaja maswala hayo.

Isitoshe tabia zisizofaa hukashifiwa katika jamii na zilizo nzuri husifiwa. Wanajamii za Abanyala na Waswahili walilenga kutumia vitendawili ili kudhihaki tabia zisizofaa. Vitendawili vingi vilivyobuniwa vilikashifu tabia za Wazungu wakoloni na Waarabu waliotamalaki janibu za jamii hizi.

Fauka ya hayo, utafiti huu ulitambua kwamba vitendawili vilitumiwa kama njia ya kusawiri maisha ya jamii za Abanyala na Waswahili. Kutokana na vitendawili vya Abanyala na Waswahili, ilibainika kwamba Abanyala hupitia hatua ya kupasha tohara ndipo vijana

(wawulana) wawe watu wazima. Vilevile swala la ukulima wa mahindi na ndizi lilijitokeza katika jamii hizi kupitia kwa vitendawili vyao vilivyoashiria vyakula hivyo ndiposa mhimili wa nadharia inayoongoza utafiti huu ikaeleza kuwa, ishara huwakilisha vashiriwa fulani. Uhusiano kati ya ishara na viashiriwa, hujengwa na dhana zilizomo akilini.

Mbali na sababu hizo zilizoelezwa, iligunduliwa kwamba vitendawili vilitumiwa katika mawasiliano kama mbinu ya kuwasilisha ujumbe kwa muhtasari. Jamii hukumbwa na maswala mazito mazito kama vile umoja, magonjwa, ambayo hayawezi kuelezwa kwa haraka na uwazi, swala la umoja katika jamii lililitiwa maanani katika vitendawili vya jamii hizi.

Vilevile, vitendawili katika jamii hizi vilitumiwa kama burudani. Burudani yenyewe ilitokana na hali kuwa wanaoshiriki katika utegaji na uteguzi wa vitendawili, hujitolea kushiriki bila ya kushurutishwa. Isitoshe, kupata au kukosa jibu katika utegaji na uteguzi wa vitendawili hakuna kuadhibiwa. Kwa ajili hiyo, wengi hushiriki katika vitendawili ili waburudishwe.

Kwa ajili ya sababu hizi, Abanyala na Waswahili hutumia vitendawili katika mawasiliano yao. Sura inayofuata imeshughulikia hitimisho la utafiti.

## SURA YA TANO

### HITIMISHO

#### 5.0 Utangulizi

Katika sura hii muhtasari wa sura ya pili, tatu na nne zimetolewa. Matokeo ya utafiti huu na mchango wake pia yameelezwa katika sura hii. Matatizo yaliyomkumba mtafiti wakati wa kufanya utafiti huu, yamezingatiwa katika sura hii. Mapendekezo ya tafiti za baadaye yametolewa ili kukikuzi kitengo hiki cha fasihi simulizi. Mwishoni hitimisho limetolewa.

#### 5.1 Muhtasari

Sitiari ni msingi wa kufichwa kwa maana ambayo msikilisaji anapaswa kutegua. Kuficha huko hutokea kitu kinapopewa jina la kitu kingine kwa mujibu wa kufanana kwa vitu hivyo. Utafiti huu ulitambua kwamba sitiari ni za aina nyingi. Ndio maana katika sura ya pili, mtafiti aliweza kubainisha sitiari zilizo katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Sitiari zilizobainishwa katika sura hiyo ni kama vile sitiarifiche, sitiari shehenezi, sitiari tashhisi, sitiari changanyi, sitiari thabiti, sitiari changamano na sitiari dhanifu. Katika sura ya tatu mtafiti alibainisha maudhui katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Katika sura ya nne mtafiti alichunguza sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao. Sura ya tano ni hitimisho.

#### 5.2 Matokeo ya utafiti

Katika sura ya pili, utafiti huu uliweza kubainisha sitiarifiche, sitiari shehenezi, sitiarififi, sitiari tashhisi, sitiari changanyi, sitiari thabiti, sitiari changamano na sitiari dhanifu katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili.

Sitiarifiche ni tamathali ya usemi inayolinganisha vitu viwili kwa uhusiano wa mbali ambapo wazo linalojitokeza huwa mbali kwa kawaida. Baadhi ya mifano ya sitiariifiche iliyotawala katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili ni kama vile uyoga, nyuki au nyigu, barabara, chawa na ugali. Uyoga ulitumiwa kurejelea sitiari ya babu aliyesimama kwa mguu mmoja, nyuki ama nyigu walitumiwa kama sitiariifiche ya watoto, kamba ilitumiwa kama sitiariifiche ya barabara na chawa akatumiwa kama kiashiriii cha ndege au Bi. Mkubwa. Mifano hiyo ilitambuliwa kwa mujibu wa mhimili unaoeleza kwamba ishara huwakilisha viashiriwa fulani. Na uhusiano kati ya ishara na viashiriwa, hujengwa na dhana zilizomo mawazoni.

Sitiari shehenezi ilibainishwa pia katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Hii ni aina ya sitiari inayoongoza maana na sifa za neno linalolinganishwa. Kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki, sifa bainifu za kisemantiki huwezesha mhakiki kupata picha fulani katika kazi za kifasihi kwa kuibua fahiwa za kimaana. Kwa misingi hiyo, utafiti huu uliweza kutambua kuwa baadhi ya vitendawili vya jamii hizi vilitoa maelezo ya kile kilichorejelewa. Maelezo yaliyotolewa ndiyo yaliyoiongoza hadhira hadi kwenye jibu la kitendawili. Maelezo hayo yalirejelea vitu vifuatavyo: yai, kisogo, mkanda, meko na hindi miongoni mwa vitu vingine.

Hali kadhalika sitiari tashhisi ilibainika katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Hii ni sitiari inayolinganisha tabia za watu na vitu visivyo na uhai. Baadhi ya vitu vilivyolinganishwa ni kama vile: nyanya alitumiwa kama kiashiriii cha kitanda, uchaga, na kiwavi. Mchwa wanaojenga vichuguu walilinganishwa na wanawake mafundi. Magadi (chumvi ya kiasili) ililinganishwa na msichana ambaye hajaolewa. Baba alilinganishwa na kitunguu kutokana na namna kitunguu kilivyo na sehemu mbalimbali zilizojaa kama makoti wanayovaa akina baba. Ulinganisho huo ulielezwa kwa mujibu wa mhimili unaoeleza kuwa

ishara huwakilisha viashiriwa fulani, uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni.

Fauka ya hayo, utafiti huu ulibaini sitiari thabiti katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Hii ni sitiari ya ulinganisho unaotumia vitu thabiti kuelezea dhana fulani. Kwamba matumizi ya kitu kinachofanana na wazo fulani, ndicho kinachotumiwa kueleza wazo hilo. Vitendawili vya Abanyala na Waswahili vilitumia ishara ya nyumba ndogo iliyojaa watu kuwakilisha kinywa na meno. Kaptula iliwakilishwa na nyumba yenye mlango mmoja na madirisha mawili. Ulimi ulielezwa kama kitu kilicho katikati ya miiba lakini hakichomwi.

Hali kadhalika sitiari changanyi ilibainishwa katika vitendawili vya jamii hizi. Sitiari changanyi ni matumizi ya sitiari tofauti tofauti zinazopatikana katika usemi mmoja au sentensi. Aina hii ya sitiari ilibainika kupitia kwa kitendawili kifuatacho miongoni mwa vingine vilivyotolewa: 'Damu ya simba imetawanyika lakini nzi hawathubutu kutua wakala ingawa wanaitamani sana – moto'. Katika mfano huo, moto umeashiriwa na damu ya simba. Nzi wametumiwa kama kiashirii cha watu wanaofaidika kutokana na moto ingawa wanafahamu hatari yake.

Vilevile sitiari dhanifu ilijitokeza katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Hii ni sitiari ambayo hutumia wazo moja kwa kulihusisha na lingine ili uelewa wake uwe waziwazi. Aina hii ya sitiari ilibainika kupitia kwa mifano iliyotoa mawazo yanayohusiana na upishi, mauti na ushirikiano katika jamii. Ndiposa mhimili wa nadharia inayoongoza utafiti huu ikaeleza kuwa sifa bainifu za kisemantiki humwezesha msanii kupata picha katika kazi za kifasihi kwa kuibua fahiwa za kimaana.

Kwa hivyo, utafiti huu uliweza kubainisha sitiari mbalimbali zinazopatikana katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Nazo ni kama vile: sitiari fiche, sitiari shehenezi, sitiari fifi, sitiari tashhisi, sitiari changamano, sitiari thabiti, sitiari changanyi na sitiari dhanifu.

Mbali na kubaini sitiari zilizo katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili, mtafiti pia alibaini maudhui katika vitendawili vya jamii hizo. Maudhui hayo yalielezwa kwa mujibu wa mhimili wa nadharia inayoongoza utafiti huu. Mhimili huo unajengwa kutokana na viashirii vya utamaduni unaorejelewa na tajriba ya maisha. Urejelezi huo huunda uhalisi mahsus kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo kuipa kazi fulani nguzo za kitamaduni. Ndiyo maana kiashirii huweza kuwa kilekile bali kinachoashiriwa kikawa tofauti kwa mujibu wa utamaduni na tajriba ya maisha.

Utafiti huu ulitambua kuwa sitiari katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili zina maudhui fulani na ndizo sababu zilizowafanya kutumia sitiari katika vitendawili vyao. Baadhi ya sitiari zilitumiwa kama kiashirii cha magonjwa na kifo. Kwa mfano sitiari ya zimwi ilitumiwa kuashiria ugonjwa hatari wa UKIMWI. Tunda aina ya fenesi liliashiriwa na mgonjwa wa ndui. Sitiari za jani kuanguka kutoka mtini lilitumiwa kuonyesha kwamba wakati mtu anapofariki hawezi kurudi.

Vilevile sitiari zilitumiwa kama kiashirii cha kuwepo kwa mifumo ya kihistoria iliyoshudia majilio ya wageni. Wageni waliozuru nchi ya Kenya kwa wakati huo walikuwa Wareno, Waajemi, Wagriki, Wazungu na Waarabu miongoni mwa wengine. Kuja kwa wageni hao kuliambatana na mjo wa vyombo vigeni kama vile: kauri, hariri, vifaa vya vita na kadhalika. Kuja kwa vyombo hivyo kulisababisha kubuniwa kwa vitendawili vyenye sitiari zilizolinganishwa navyo. Fauka ya hayo, chanzo cha funza nchini kinaamiwa kilitokana na

Wazungu wakoloni, hatua hiyo ilifanya jamii hizi kuunda vitendawili vyenye sitiari kama kifuatacho: ‘mzungu ananitekenya - funza’ iliyoashiria funza.

Isitoshe sitiari zilitumiwa katika vitendawili kama kiashirii cha sayansi ya mazingira, sitiari mbalimbali katika vitendawili zilionyesha jinsi waja wanavyokabiliana na mazingira yanayowazunguka. Baadhi ya sitiari hizo ni kama vile ‘baba’ alitumiwa kuashiria mvua, sitiari zingine zilirejelea ujauzito ambao huwa fumbo kwa sababu mtoto ambaye hajazaliwa huwa haijulikani ni wa jinsia ipi na atazaliwa lini? Sitiari zingine zilitumiwa kurejelea jua, mwezi na nyota.

Mchapuko wa kiteknolojia ulianza katika mataifa ya bara Uropa na baadaye katika nchi nyingi za bara Afrika. Mchapuko huo ulisababisha kuundwa kwa sitiari mbalimbali zilizoonyesha baadhi ya vitu vilivyokuwepo kwa wakati huo. Sitiari zizo hizo, ndizo zilizotumiwa katika vitendawili vya Abanyala na Waswahili kuashiria hali hiyo. Kwa mfano ‘watwana wasiolalamika’ waliwakilisha mitambo. ‘Watoto wasiokamatana’ waliashiria magurudumu na ‘gari lilojaa chuma’ liliwakilisha njiti. Kwa ajili hii, sitiari zilitumiwa kuonyesha mchapuko wa kiteknolojia.

Sitiari vilevile zilitumiwa kama kiashirii cha chakula, ilitambuliwa kwamba ugali, ndizi, viazi na mihogo ni miongoni mwa vyakula vilivyoliwa na jamii hizi. Kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki, ishara huwakilisha viashiriwa fulani na uhusiano kati ya ishara na viashiriwa hujengwa na dhana zilizomo mawazoni. Kwa hivyo, ishara ya mlima katika baadhi ya vitendawili vya jamii hizi ilionyesha ugali. Ishara ya ng’ombe waliolala na mkia nje na beberu mkubwa walionyesha viazi. Ni bayana kwamba sitiari zinazotumiwa katika

vitendawili vya Abanyala na Waswahili zina maudhui mengi. Hii inatokana na mifano ya vitendawili vilivyodondolewa kutokajamii hizi.

Utafiti huu pia ulitambua kwamba kuna sababu zinazowafanya Abanyala na Waswahili kutumia vitendawili katika mawasiliano yao. Miongoni mwa sababu hizo ni kuchochea udadisi, kukuza maadili, kuelimisha, kudhihaki, kuonyesha hali yao ya maisha, kuburudisha na kutumiwa kama njia ya kuwasilisha muhtasari wa ujumbe.

Uzoefu wa kutafuta kiini cha kitendawili ambao hujenga tabia ya kutaka kufichua jambo lililofichika katika kitendawili huchochea udadisi miongoni mwa wanajamii. Mfumo wa kuuliza swali na kungojea jibu, huwachochea hadhira kufaraghua katika mazingira yao ili waweze kupata jibu la kitendawili kilichotegwa. Hali hii imevifanya vitendawili kuwa kichocheo cha udadisi.

Jamii za Abanyala na Waswahili zilitumia vitendawili ili kukuza maadili. Hali hii iliwezekana kupitia kwa utaratibu maalum unaostahili kufuatwa wakati wa kutega na kutegua vitendawili. Hii ilikuwa njia moja ya kuadilisha, hali kadhalika vitendawili vya jamii hizi vilikashifu uhusiano wa kimapenzi kati ya mandugu – ‘Nyumbani mwetu kuna papai lililoiva lakini nashindwa kulila – kaka hawezi kumwoa dadake.’ Pia mienendo hasi kama maringo, yalikataliwa kupitia kwa vitendawili vyao.

Vitendawili vya jamii hizi vilitumiwa kama chombo cha kuelimisha. Wanajamii walielimishwa namna ya kuhesabu, sehemu za mwili, ushirikiano, sayansi ya kimazingira miongoni mwa maswala mengine. Haya yaliwezekana kupitia kwa vitendawili vyao vilivyohusisha maswala hayo.

Ilitambuliwa kwamba kupitia kwa vitendawili, jamii hizi za Abanyala na Waswahili waliweza kuwadhihaki baadhi ya wageni waliotangamana katika janibu zao kama vile Wazungu wakoloni. Vitendawili tofauti tofauti vyenye sitiari zilizowarejelea ziliundwa ili kuwadhihaki wageni hao. Kwa mfano, 'Mwaarabu wangu ametupwa miibani – machicha ya nazi,' 'Mzungu wangu katupwa jalalani – machicha ya nazi.'

Mbali na hayo, utafiti huu ulibaini kuwa vitendawili vilitumiwa kama kigezo cha kusawiri maisha ya jamii. Kupitia kwa vitendawili vya jamii za Abanyala na Waswahili, hatua anazopitia mtoto mvulana ndipo aingie katika hatua ya utu uzima ilielezwa kupitia kwa vitendawili vyao. Vitendawili vyao vilionyesha kuwa kisu cha ngariba ni kikali mno ndiposa kikalinganishwa na pilipili manga. Hali kadhalika ilitambuliwa kwamba jamii hizi hujishughulisha na upanzi wa mahindi, mihogo, viazi na kadhalika kupitia kwa vitendawili vyao.

Kutokana na utafiti huu, ilidhihirika kuwa vitendawili huburudisha jamii kwa ujumla. Mbali na kuwa vitendawili vinatahiniwa shuleni katika mitihani ya kitaifa, vitendawili viliwaburudisha wengi. Hii ni kwa sababu utegaji na uteguzi wavyo hujikita katika mfumo maalum wa swali na jibu. Vilevile, wale wanaoshiriki hawashurutishwi, wao hushiriki katika shughuli hiyo ya kutega na kitegua kwa hiari yao. Fauka ya hayo, kupata na kukosa jibu la kitendawili, hakuna kuadhibiwa zaidi ya kutoa zawadi ya mji, kwa njia hizo hadhira huburudika barabara.

Sababu nyingine iliyotambuliwa ni kwamba vitendawili vilitumiwa kama njia ya kuwasilisha ujumbe kwa muhtasari. Siku hizi, jamii imekumbwa na maswala mazito mazito kama vile magonjwa na umoja wa kitaifa. Kusema maswala hayo hadharani kwa wakati mwingine

huzua aibu ama uhasama. Hali hii imepelekea vitendawili vyenye sitiari zinazotaja maswala hayo kutumiwa katika mawasiliano.

### **5.3 Mchango wa utafiti**

Vitendawili kama sehemu ya masimulizi yetu, ni amali muhimu za jamii zetu. Kwa ajili hiyo, utafiti huu ni wenye manufaa kwani unatoa mchango mkubwa kwa tafiti zilizofanywa na zitakazofanywa katika kitengo hiki cha vitendawili. Kipera hiki cha fasihi simulizi hutahiniwa katika mitihani ya kitaifa ya darasa la nane na kidato cha nne. Kwa hivyo utafiti huu utawafaidi wanafunzi na walimu kwa kuwapa uelewa zaidi kuhusu sitiari na umuhimu wake katika vitendawili.

Isitoshe, njia maarufu ya mawasiliano hivi leo ni kupitia kwa vitendawili. Kwa ufundi wake wa matumizi yake ya sitiari, wengi wameweza kueleza jambo zito likaonekana kuwa jepesi. Kwa sababu hiyo, kitengo hiki cha fasihi simulizi kitasaidia kuboresha mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Kwa hivyo, utafiti huu utakuwa wenye manufaa kwa jamii nzima.

Kwa ambavyo lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa hapa nchini, utafiti wa aina hii huikuza lugha ya Kiswahili na kujenga utamaduni wa taifa. Vilevile tafiti za sampuli hii zitaonyesha kwamba sanaa ya vitendawili ina dalili za kukua na kukomaa tofauti na ilivyodaiwa kwamba sanaa hii inaonyesha dalili za kudumaa.

### **5.4 Changamoto za utafiti**

Shughuli ya utafiti hukumbwa na matatizo tofauti tofauti, hata hivyo uvumilivu, bidii na ari aliyokuwa nayo mtafiti, ilifanya utafiti huu kuendelea. Mtafiti alikumbwa na matatizo ya kijamii ambapo wanajamii wengi hawakujitolea kushiriki katika utafiti huu. Baadhi yao

waliona kuwa lilikuwa ni jambo la kuwapotezea muda ilipokuwa wakati wa kukusanya data. Isitoshe wale waliokubali kushiriki, walitarajia malipo hata hivyo mtafiti aliweza kusuluhisha matatizo hayo kwa kuwa na waelekezi.

## **5.5 Mapendekezo**

Kutokana na utafiti huu, mtafiti anapendekeza maswala yafuatayo kufanyiwa utafiti zaidi ili kukirutubisha kipera hiki cha fasihi simulizi.

1. Ipo haja ya kutazama umuhimu wa maudhui ya vitendawili katika kuimarisha dhima yake.
2. Kuna haja ya kuchunguza uhusiano wa vitendawili na methali za Kiswahili.
3. Kutazama umuhimu wa sitiari katika vipera vingine vya fasihi simulizi kama vile nyimbo.

## **5.6 Hitimisho**

Kutokana na utafiti huu, ni bayana kuwa kuna mlingano mkubwa kati ya vitendawili vya Abanyala na Waswahili. Swala hilo lilijitokeza kupitia kwa sitiari zilizobainika katika vitendawili vya jamii hizo mbili. Pia sitiari hizo zina maudhui yanayopelekea kutumiwa kwazo katika vitendawili vya jamii hizo. Mbali na hayo, wanajamii wa Abanyala na Waswahili, wana sababu mbalimbali zinazowafanya kutumia vitendawili katika mawasiliano yao, baadhi ya sababu hizo ni kama vile: kuchemsha bongo, kudhihaki, kuelimisha, kuonyesha hali halisi ya maisha yao, kukuza maadili, kuburudisha na kutumiwa kama nia ya kuwasilisha ujumbe kwa muhtasari.

Utafiti huu utakuwa wenye manufaa kwa kutoa mchango mkubwa kwa tafiti zilizofanywa na zitakazofanywa katika kitengo hiki na fasihi simulizi kwa ujumla. Isitoshe utafiti huu utasaidia uelewa wa kipera hiki cha utanzu wa semi wa fasihi simulizi. Fauka ya hayo, kwa

ufundi wake wa matumizi ya sitiari, utanzu huu utaboresha zaidi mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Kwa hivyo utafiti huu utakuwa wenye manufaa kwa jamii nzima.

## MAREJELEO

Ahadi Kenya Trust (2012). "Origin of Jiggers." [www.jigger.ahadi.org.faq.html](http://www.jigger.ahadi.org.faq.html)

Tarehe 13.9.2013.

Akivaga, K. na Odaga, B. (1982). *Oral Literature: A School Certificate Course*. Heinemann Educational Publishers. Nairobi

Amana, B. (2013). *Vitendawili*. <http://EducationKenya.blogspot.com/>

Barthes, R. (1977). "Image, Music and Text." Richard Howard (Tran) katika David H.

Richter (Mhariri). *The Critical Tradition: Classical and Contemporary Trends*.

New York. Bedford Books.

Beuchart, P.D. (1965). "Riddles in Bantu." Katika, *The Study of Folklore*. New Jersey. 16, 3

Uk.133-149. Routledge. Taylor and Francis Group.

Blacking, J. (1961). "The Social Value of Venda Riddles." katika *Africa Studies*. Toleo

Na. 20, 1: Uk.1-32. Routledge. Taylor and Francis Group.

Culler, J. (1981). *The Pursuit of Sign: Semiotics, Literature and Deconstruction*. Ithaca

University Press: Ithaca N.Y. Cornell.

Chacha, D.M. (1991). "Kitendawili cha Vitendawili: Maana na Matumizi katika Jamii

ya Wakuria," *Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Kenyatta*.

Chesaina, C. (1991). *Oral Literature of the Kalenjin*. East African Educational Publishers.

Nairobi.

Eschbach, A. (1983). *Foundations of Semiotics*. Amsterdam: John Benjamin's Publishing

Company.

Farsi, S.S. (1958). *Swahili Sayings from Zanzibar*. Kenya Literature Bureau. Nairobi.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Oxford University Press. Nairobi.

Gatimu, L.N. (2012). "Umenke na Ubaguzi wa Kijinsia Katika Methali na Vitendawili vya

Kiswahili.” <http://erepository.uobi.ac.ke:8080/xm/ui/handle/123456789/8986>

Tarehe 1.4.2013.

Gibbs, R.W. (1994). *The Poetics of Mind: Figurative Thought, Language and Understanding*. Cambridge University Press

Hamad, A.K. (1981). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni. Dar es Salaam.

Hamnet, I. (1967). “Ambiguity, Classification and Change: The Function of Riddles.” Katika *Man*. Toleo la 2.

Harries, L.(1942). “Makua Song Riddles from Initiation Rites.” katika *African Studies*. Toleo la 1. Nambari 1. Austin: University of Texas Press.

Harries, L. (1947). “Some riddles of the Mwera People.” katika *African Studies*. Toleo 6. Nambari 1. Austin: University of Texas Press.

Hedley, J. (1998): *Power in Verse: Metaphor and Metonymy in the Renaissance Lyric*. London: The Pennsylvania State University press.

Inama, A. (2012). ‘Map of Navakholo Constituency.’ <http://www.flickr.com/>

Innis, R.E. (1985). *Semiotics*. London: Indiana University Press.

Kabira, M. W. (1988). *Gikuyu Oral Literature*. Heinemann Kenya. Nairobi.

Kallen, J. na Carol, M. (1979). *Structure & Meaning in Kiswahili Riddles*. Journal of American Folklore 92/386 (September- December 1979): 418-44.

Kasomo, D. (2006). *Research Methods in Humanities and Education*. Kijabe Printing Press. Egerton University Press.

Kenya Information Guide (2013). “Kenya’s Second Largest Ethnic Tribe.”

<http://www.kenya-information-guide.com/index.html> Tarehe 9.9.2013 saa 6:27 jioni

King’ei, K. na Kisovi, M.N.C. (2005). *Misingi wa Fasihi Simulizi*. Kenya Literature Bureau. Nairobi.

- Kipury, N. (1983). *Oral Literature of the Maasai*. Heinemann Educational Books. Nairobi.
- Kiruthu, F. na wengine (1996). *The Evolving World: A History and Government Course*.  
Form 2. Oxford University Press, East African Ltd. Nairobi.
- Kobia, J.M. (2008). "Metaphors on HIV/AIDS Discourse among Oluluyia Speakers of  
Western Kenya." <http://cadaad.org/ejournal> vol 2 (2): 48-66.
- Kombo, K.D. na Tromp, A.L.D. (2006). *Proposal and Thesis writing: An Introduction*.  
Pauline Publications Africa.
- Lakoff, G. na Johnson, M. (1980). *Metaphors We Live By*. University of Chicago Press.  
Chicago
- Lambert, H. E.(1962/3). "Some Riddles from the Southern Kenyan Coast." katika Knappert,  
J.(mhariri). *Swahili*. I.T.L.C. Amazon. com
- Maitaria, N.J. (2012). "Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili: Dhima ya Methali." Tasnifu ya  
Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Mazrui na Syambo, B. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. East African Educational Publishers.  
Nairobi.
- Mbaabu, I. (1978). *Methali, Vitendawili na Mashairi ya Kimeru*. Nairobi. K.L.B
- Miruka, O. (1994). *Encounter with Oral Literature*. East African Educational  
Publishers. Nairobi.
- Momanyi, C. (2006). "Dhima na Utendakazi wa Vitendawili Katika Jamii," katika Njogu, K.  
( na wengine wahariri) *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Twaweza Communications.  
Nairobi. Uk.19-28
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. East African Educational Publishers  
Nairobi.
- Murdoch, J. (2008). "The Truth about Lies." <http://www.fvbooks.com/jmurdoch6.htm>

- Mugenda, O.M. na Mugenda, A.G. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*: Acts Press.
- Nakunga,(2011). “Vitendawili” <http://nakunga.Blogspot.Com/2011/07/Vitendawili.html>
- Nandwa, J. (1976). “Oral Literature among the Abaluyia” Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Ndirangu, D.M. (2011). “Kenya’s Indigenous Radio Stations and their uses of Metorphors in 2007ElectionViolence.”  
<http://www.ingentaconnect.com/content/intelect/jams;jsessionid=13b7okf5hp8u6.alice>
- Ndungo, C. (2006). “Matumizi ya Tamathali za Usemi katika Lugha ya Kisiasa”  
Katika Njogu, K. na wengine (wahariri) *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Twaweza Communications. Nairobi. Uk.107-11
- Ngonyani, D.E.O. (2005). “Vitendawili vya Kiswahili: Usambamba wake na Dhima yake Katika Jamii.” <http://www.qucosa.de/fileadmin/data/qucosa/documents/9831/12-10-Ngonyani.pdf> tarehe 13.07.2013
- Nordquist, R.(2013). “What are Mixed Metaphors?”  
<http://grammar.about.com/bio/Richard-Nordquist-22176.htm>
- Nzookwa, C. J. (2011). “Dokezo za sitiari katika Methali za Kiswahili na Kiganda.”  
<http://mak.ac.ug/documents/Makfiles/theses/Nzookwa-John.pdf>
- Nyanchama, B. M. (2004). “Matumizi ya Taswira na Ishara katika Sauti ya Dhiki,”  
Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta.
- Ochieng, W.R. (1985). *A History of Kenya*. Macmillan Publishers Ltd.  
London and Basingstoke.

- Omari, C.K. (na wengine) (Wahariri) (1975). *Misemo na Methali Toka Tanzania*. East Africa Literature Bureau. Nairobi.
- P'Bitek, O. (1973). *Africas Cultural Revolution*. Heinemann Educational Publishers. Nairobi.
- Pierce, C. (1977). *Semiotics and Significs*. Indiana University Press. Bloomington.
- Richards, S. (1965). *Semantics*. Newyork. MacGraw Hill Book Company.
- Roberts, B. (1970). *Semantics and Language Analysis*. New York. Bobbs. Merrill Company Library U.S.A
- Royle, N. na Andrew (1995). *Introduction to Literature Criticism and Theory*. Pearson Education Ltd. London.
- Saussure, de F. (1974). *Course in General Linguistics*. Fontana. London.
- Senkoro, F.E.M.K. (1982). *Fasihi*. Press and Publicity Centre. Dar es Salaam.
- Scholes, R. (1974). *Structuralism in Literature*. Yale University Press. New Haven.
- Scotts, T.C. (1965). Persian and Arabic Riddles: A Language – Centered Approach to Genre Definition.” Bloomington: Indiana University.
- Steffies (2013). “The 15 Types of Metaphor”  
<http://steffiesstoryboard.blogspot.com/2013/02/different-types-of-metaphors-and-examples.html>
- Todoli, J. (2007). “Disease Metaphor in Urban Planning.” *Katika Critical Approaches to Discourse Analysis across Displines*. 1 (2) 51-60.
- Trang, T. (2013). “An Investigation into Stylistic Devices Commonly used in Riddles: English vs Vietnamese.” <http://kngoangu.duytan.edu.vn/Home/categoryDetail/vn/94/de-tai-nghien-cuu>
- Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. The Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi.

## VIAMBATISHO

(i) **Kiambatisho cha maswali ya mahojiano kwa wazee wa jamii ya Abanyala wenye umri wa miaka kati ya 65- 80.**

(a) Abanyala wana njia mbalimbali za kuwasiliana? .....

(b) Vitendawili ni mojawapo ya njia hizo? .....

(c) Tega kitendawili kimoja unachokijua na ukitegue.....  
.....

(d) Kitendawili hicho kinataja majina yapi? .....

(e) Kwa nini majina hayo yakatumiwa? .....

(f)Ujumbe wa kitendawili hicho ni nini? .....

(g)Je, ni nini kitakachokufanya umtegee mtu kitendawili hicho? .....

(ii) **Kiambatisho cha maswali ya mahojiano kwa wazee wa jamii ya Waswahili wenye umri wa miaka kati ya 65-80**

(a) Waswahili wana njia mbalimbali za kuwasiliana? .....

(b) Vitendawili ni mojawapo ya njia hizo? .....

(c) Tega kitendawili kimoja unachokijua na ukitegue.....  
.....

(d) Kitendawili hicho kinataja majina yapi? .....

(e) Kwa nini majina hayo yakatumiwa? .....

(f) Ujumbe wa kitendawili hicho ni nini? .....

(g) Je, ni nini kitakachokufanya umtegee mtu kitendawili hicho? .....

**(iii) Kiambatisho cha maswali ya mahojiano kwa watoto**

Tega kitendawili kimoja kimoja kinachohusu mambo yafuatayo:

(i) Ndege.....


(ii) Wanyama.....

(iii) Mimea.....

(iv) Uongozi.....

(v) Teknolojia.....

(iv) Kiambatisho eneo la Abanyala (Navakholo)



(v) Kiambatisho cha eneo la Mombasa mji wa Kale



Kwa hisani ya looked up [www.paged2.google syndication.com](http://www.paged2.google syndication.com)